# Nipashe

Alhamisi Januari 9, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580123

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





## Shahidi asimulia kortini alivyobakwa na mkimbizi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Vyeti vya kuzaliwa vyamwibua waziri

• **Ni** kuhusu kutumika kuandikisha watoto shule, apiga 'stop' walimu kuwadai wazazi...*Endelea ukurasa 22*



Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), Halima Mdee, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mbivu, mbichi Meya Dar leo

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Vigogo taasisi 36 njia panda

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAZIFUTA AZAM, MTIBWA Z'BAR UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri: Vigogo taasisi 36 wasiende ofisini Jan 24

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema wenyeviti wa bodi na wakurugenzi wa taasisi 36 ambazo hazijawasilisha gawio kwa serikali, wasiende ofisini Januari 24 mwaka huu kwa kuwa uteuzi wao utakuwa umeshatenguliwa.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapa baada ya kupokea gawio la zaidi ya Sh. bilioni 500 kutoka kwa taasisi, mashirika na kampuni 13.

Alisema anawashukuru na kuwapongeza wenyeviti na wakurugenzi wa bodi waliotii maagizo yaliyotolewa na Rais John Magufuli kuhakikisha wanatoa gawio kwa serikali na kusema kuwa hilo siyo jambo dogo.

"Hatuna mjomba na hayupo, na viongozi wetu walianzisha jambo hili kwa kuwa walikuwa wanajua kuna sehemu serikali imewekeza fedha zake, hivyo ni muhimu gawio hilo kutolewa.

Ukiangalia kama Shirika la Utangazi la Taifa (TBC), mwaka wa 10 huu Watanzania ndiyo wanapata chochote kwa mara ya kwanza, pia tumekuwa na vyuo vyetu ambavyo najua kuwa vina mahitaji makubwa, lakini tunajua kuwa kuna watafiti wanakuja na kuingiza kidogo, hivyo hicho kinachopatikana ni muhimu kikatolewa kwani kinaweza kusaidia kutoa mikopo kwa wanafunzi.

"Nawashukuru sana kwa niaba ya serikali na ni matarajio yangu kuwa mwaka ujao, mtawekeza zaidi na zaidi. Misaada siku hizi duniani imepungua, na tutaendelea kutegemea misaada mpaka lini? Yaani unakuwaje mwenyekiti wa bodi halafu unashindwa kuleta kile ambacho Rais ameagiza?

"Taasisi 36 zilizobaki, wenyeviti wa bodi pamoja na wakurugenzi ifikapo saa sita usiku Januari 23 mwaka huu, kama hawajaleta gawio, wajitoe, waachie madaraka yao na hata wasingoje kuleta barua kwangu na hili ninaongea kwa mara ya mwisho, sitarudia tena.

"Katika hili hatutanii, Watanzania milioni 55, hatutakosa wenyeviti wa bodi na wakurugenzi, tena vijana wazuri kabisa ambao wanaweza kufanya kile wanachoagizwa? Hivyo, wale waliobaki niwaambie kuwa hakuna utani katika hili," alionya.

Waziri huyo alisema anajivunia makusanyo ya serikali ambayo

INAENDELEA UK.8



Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na maspika wenzake, katika Mkutano wa Maspika na Viongozi wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, uliofanyika katika Bunge la Canada, jijini Ottawa jana. Kutoka (kulia) ni Spika wa Bunge la Ghana, Michael Oquaye, Spika wa Bunge la Uganda, Rebecca Kadaga, Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi, Spika wa Kisiwa cha Man, Juan Peterson na Spika wa Bunge la Pili la Kisiwa cha Man, Steve Rodan. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Mbivu, mbichi Meya wa Dar leo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imepanga kutoa uamuzi wake leo wa kisitisha mchakato wa kumvua umeya, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, au la.

Mwita aliwasilisha jana kiapo chini ya hati ya dharura kuzuia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuendelea na mchakato wa kumwondoa kwenye kiti cha umeya mpaka kesi ya msingi itakaposikilizwa.

Uamuzi huo unatarajia kutolewa leo na Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Mtega, aliyesikiliza maombi madogo ya mlalamikaji.

Mwita amefungua maombi ya msingi kupitia Wakili Hekima Mwasipu dhidi ya walalamikiwa watatu ambao ni Halmashauri ya Jiji, Makonda na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwasipu alidai kuwa maombi ya msingi yamepangwa kwa ajili ya kutajwa lakini mlalamikaji ana maombi madogo mawili.

Alidai, mlalamikaji amewasilisha maombi hayo chini ya hati ya kiapo cha dharura na yanalenga kuwazuia Mkuu wa Mkoa na Halmashauri kujihusisha katika mchakato wa kumng'oa kwenye nafasi ya umeya.

"Mheshimiwa hakimu mlalamikaji anaiomba mahakama izuie mchakato huo au hata kama kutakuwa na kikao kisijadili mambo mengine ya maendeleo na kwamba kuhusu kumng'oa kwenye kiti chake ajenda hiyo isizungumziwe na Mkuu wa Mkoa pamoja na halmashauri wazuiwe kufanya mchakato huo," alidai na kuongeza.

"Mahakama isipowazuia walalamikiwa wa kwanza na wa pili, mlalamikaji hatapata haki yake ya kusikilizwa," alidai Mwasipu.

Akijibu hoja hiyo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, alidai kesi hiyo imekuja kusikilizwa chini ya hati ya dharura ili haki ionekane imetendeka.

Alidai hawajui kama kuna kitu chochote kinachoweza kutokea kuhusu kung'olewa kwa mleta maombi huyo, hivyo aliiomba mahakama kukataa maombi hayo kwa gharama.

Malata alidai hakuna mazingira ya moja kwa moja yanayoashiria kwamba kwenye kikao kitakachofanyika kutakuwa na ajenda inayohusu kumtoa katika nafasi hiyo meya huyo.

Hata hivyo, jopo la mawakili wa serikali tayari limewasilisha mapingamizi kupinga maombi ya msingi yaliyopo mahakamani hapo.

Hakimu Mtega aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya kutoa uamuzi wa ama kusitisha mchakato huo au la.

## Mvua yakwamisha usafiri vifaa ujenzi reli ya kisasa

**Na Idda Mushi,** KILOSA

VIFAA vinavyotumika katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Kilosa mkoani Morogoro, vimekwama kufika eneo la ujenzi kutokana na kukatika kwa mawasiliano ya barabara ya Chanzuru-Junction-Melela inayokwenda wilayani Kilosa.

Imeelezwa kuwa mvua inayoendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro, imesababisha kujaa maji kwa barabara hiyo na kusababisha usumbufu kwa watumiaji na wakiwamo makandarasi wanaojenga reli hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alifika kwenye eneo hilo lililojaa maji ili kushughulikia tatizo hilo jana, na katika hatua za awali akawashauri wasimamizi wa mradi huo mkubwa kutumia vifaa vyao kusaidia utatuzi wa muda, kuondoa maji hayo kwa kuwa tayari barabara hiyo iko kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Morogoro na Katibu Tawala wa Mkoa kuomba fedha za dharura Serikali Kuu, ili zitumike kujenga barabara ya kilometa tatu kwa kiwango cha lami katika eneo hilo, huku akikiri kunahitajika fedha za kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 61 ili kukabiliana na mafuriko.

"Hizi kilometa tatu zimekuwa na shida ya mara kwa mara ya mafuruko pindi mvua zikinyesha, hata kwenye mikoa ya jirani ikiwamo Dodoma na Manyara, hivyo ni lazima Tanroads mharakishe kuomba fedha ili kutengeneza eneo hili kwa dharura," aliagiza.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoyi, alisema barabara hiyo iko chini, hivyo kuhitaji tuta kuiinua na kujengwa makalavati mengi kwa vile wilaya hiyo imekuwa ikiathiriwa zaidi na maji ya mafuriko.

Kaimu Meneja waTanroads Mkoa wa Morogoro, Godwin Andaluwisye, aliahidi kufanyia kazi maagizo ya mkuu wa mkoa, akieleza kuwa eneo hilo liko bondeni na limekuwa likichukua maji ya mvua kutoka Mikumi na Kilosa pindi mvua inaponyesha mikoa ya Dodoma na Manyara.

"Maji yakija, yanasababisha uharibifu wa barabara na makalavati yaliyopo, lakini tumepokea maelekezo na tunafanyia kazi ingawa tayari barabara hii imeshafanyiwa usanifu kwa ajili ya kuwekwa lami kutoka Melela hadi Kilosa na kuelelea Mikumi," aliahidi.

## HABARI KITAIFA



Mwendesha boda-boda akiwa amewapakia wanafunzi wanne maarufu mshikaki, huku wote wakiwa hawajavaa kofia ngumu katika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao na uvunjifu wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Matatani kwa tuhuma za kumteka raia wa Marekani

**Na Rahma Suleimaan,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja linamshikilia kijana Seif Salum Machano (28), mkazi wa Bububu Unguja kwa tuhuma za kumteka mtalii ambaye ni raia wa Marekani na kumwibia.

Kijana huyo akiwa na wenzake wanne ambao hawajapatikana, wanadaiwa kumteka mtu huyo, Sheiley Moris Brandjester, ambaye yupo Zanzibar kwa matembezi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Juma Haji, alisema mtuhumiwa huyo akiwa na wenzake walimteka raia huyo eneo la Darajani Mjini Unguja wakati akitafuta usafiri wa kuelekea Michamvi Mkoa wa Kusini Unguja kwa ajili ya matembezi.

Kamanda Haji alieleza kuwa mtuhumiwa huyo akiwa na wezake katika gari aina ya Noah yenye namba Z419 GV, walimlaghai mtalii huyo na kumwahidi kuwa watampeleka katika safari yake ya kuelekea Michamvi.

Alieleza kuwa mtuhumiwa huyo na wenzake walimpeleka Brandjester eneo la Kwarara badala ya Michamvi kama walivyomwahidi, na kumtaka atoe kila kitu alichonacho ili kuokoa maisha yake.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa katika mashine ya kutolea pesa (ATM) eneo la Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini Magharib Unguja alipoenda kutoa fedha.

Alisema alipokamatwa katika ATM ilikutwa na kadi ambayo si ya kwake, hivyo kushindwa kutoa fedha ndipo alipojieleza na kuongozana na askari polisi hadi eneo la tukio kwa ajili ya kuwabaini wenzake wanne.

Kwa mujibu wa Haji, watuhumiwa wenzake ambao hawajatambulika, walifanikiwa kukimbia na kumuacha raia huyo akiwa katika gari

INAENDELEA UK.8

# Mwanamke asimulia kortini alivyobakwa na mkimbizi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

SHAHIDI wa kwanza katika kesi inayomkabili mkimbizi wa Kambi ya Nyarugusu, raia wa Jamhuri ya Kidemokraia ya Congo (DRC), Ramadhani Salum (44), jana alieleza mahakama mshtakiwa alivyombaka anayekabiliwa na shtaka la kubaka.

Salum anadaiwa kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 39 (jina linahifadhiwa), mkimbizi wa kambi ya Nduta, raia wa Burundi, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Mshtakiwa huyo alifikishwa hapo mahakamani jana akitokea mahabusu katika Gereza la Bangwe na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Katoki Mwakitalu.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, shahidi hiyo alidai kuwa: "Mimi ni Mrundi naishi katika kambi ya wakimbizi Nduta, Kibondo Mkoa wa Kigoma na nina miaka 39. Nilifika katika kambi ya wakimbizi Nduta mwaka 2005."

Alidai kuwa Oktoba 4, mwaka jana, alikuwa kwenye kambi ya NMC iliyoko Kibirizi Manispaa ya Kigoma/Ujiji kwa sababu alikuwa amefika hapo kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji kwenye uzazi majira ya saa 7:00 mchana akitokea ofisi ya IRC.

Kwa mujibu wa shahidi huyo, alisikia njaa, hivyo akaondoka ili akapate chakula na kabla hajaenda kula chakula, alikaa pembeni ya mlango wa chumba anacholala peke yake, maana sehemu hiyo ina vyumba vingi vya wakimbizi wanaoumwa magonjwa mbalimbali.

Alidai kuwa wakati amekaa pembeni mwa mlango wa chumba hicho, alimwona mshtakiwa Ramadhani Salumu anakuja kwake na alipofika alimwambia: "Tupendane, mimi nikakataa. Akarudia tena kusema tupendane mimi nikasema hapana ndipo akanishika mkono na kunivuta na kunipeleka kwenye mlango wa chumba ninacholala mimi nikapiga kelele na kushika mlango ili nisiingie ndani na mlango ukabomoka."

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa baada ya kupiga kelele mshtakiwa huyo alimfumba mdomo na wakati purukushani hizo zikiendelea, watu wengine walikuwa nje ya kambi ya NMC na wengine walikuwa wamekwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa Maweni kwa ajili ya matibabu ndipo mshtakiwa huyo alipomshinda nguvu na kumtupa chumbani kwake anakolala.

Wakati wanagombana, alidai kuwa mshtakiwa alimchania gauni lake sehemu ya kifuani, kisha alipomzidi nguvu akampandisha kitandani na kumpanua miguu yake ikashindikana ndipo mshtakiwa akapiga magoti kwenye sehemu zake za nyonga ndipo akamvua nguo ya ndani ikachanika sehemu za pembeni kushoto na kulia.

"Naiomba mahakama hii ipokee nguo hii ya ndani na gauni hili ili viwe vielelezo katika kesi yangu," alidai shahidi huyo.

Aidha, Hakimu Mwakitalu alisema nguo hizo zilizochanika zimepokewa mahakamani kama vielelezo katika kesi hiyo kwa upande wa mashtaka.

Shahidi huyo alidai mahakamani kuwa mshtakiwa huyo baada ya kuchana nguo yake ya ndani, alimfinya na kumzidi nguvu akachukua uume wake na kuuingiza kwenye uke wake na wakati akiendelea kumbaka, alidai alikuwa akimnyonya ulimi na alipojaribu kupiga kelele, mshtakiwa alimfumba mdomo kwa kutumia mkono wake.

Wakati mshtakiwa anambaka ndani, alidai kuwa alisikia kishindo cha mtu anatembea ndipo mshtakiwa alipotoka juu yake na kuvaa nguo zake haraka na yeye pia akashuka kitandani haraka ili kumzuia mshtakiwa huyo kukimbia.

Aliendelea kudai kuwa baada ya muda alifika kwenye hicho chumba mama anayejulikana kwa jina la Miyongulu Yudes, akamuuliza mbona unapiga kelele na kumjibu Salum amembaka ndipo mshtakiwa huyo akapiga magoti kuomba msamaha kwa kitendo alichokifanya.

Baada ya muda, alidai alikuja Ntimbaganigwa Fides na kuelezwa yaliyotokea ndipo mshtakiwa huyo pia akapiga magoti na kuomba msamaha kwa kitendo

INAENDELEA UK.8


SERENGETI BREWERIES

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATAPELI WANAOJITAMBULISHA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA SERENGETI BREWERIES LIMITED**

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), imepokea taarifa za matukio ya utapeli kutoka kwa wamiliki wa mabaa kutoka sehemu mbali mbali nchini ambao wanalalamika kufuatwa na matapeli wanaojitambulisha kama wafanyakazi wa SBL.

Matapeli hao, wamekuwa wakiwashawishi wenye mabaa kuwapa fedha ili wawapatie viti, meza, maturubai, majokofu pamoja na vifaa vingine vya promosheni kutoka SBL. Kundi hilo lenye nia ovu, limekwenda mbali zaidi kwa kutumia vitambulisho feki vya kampuni pamoja na nembo ili kutimiza malengo yao ya kufanya utapeli.

Tunapenda kuwafahamisha wateja wetu na Umma kwa ujumla kuwa, SBL na wafanyakazi wake hawawezi kuwashawishi wenye mabaa au mtu mwingine yeyote inayofanya naye biashara kutoa fedha kwa ajili ya kupatiwa vifaa mbali mbali vya promosheni. Vifaa vya promosheni, hutolewa kwa wadau wetu wa biashara BURE kwa lengo la kuongeza muonekano wetu sokoni.

Tunapenda kuwataarifu wenye mabaa na Umma kwa ujumla kuwa makini na matapeli hao na kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama mara tu wanapowabaini.

Kampuni ya SBL haitachukua dhamana yoyote kwa vitendo au hasara itakayosababishwa na utapeli huu.

*IMETOLEWA NA UONGOZI WA KAMPUNI YA SBL*

215578302

# Mpina atatua mgogoro uliodumu kwa miaka 10

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amemaliza mgogoro wa ardhi baina ya wananchi zaidi ya 4,000 wa Kijiji cha Ngadinda na Shamba la Mifugo la Serikali la Hanga Ngadinda, uliodumu kwa zaidi ya miaka 10 na kuamua kumega hekta 1,800 zitakazogawiwa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na makazi.

Hatua hiyo ya serikali imekuja baada wananchi wa kijiji hicho kulalamikia kukosa maeneo ya kilimo na makazi kutokana na kijiji chao kuzungukwa na shamba la serikali la mifugo na wamekuwa wakikamatwa, kupigwa na kuchomewa nyumba na mazao yao.

Kabla ya uamuzi huo wa kulimega, shamba hilo la serikali lilikuwa na ukubwa wa hekta 6,147, likitumiwa kuzalisha mitamba ya ng'ombe wa maziwa.

Hata hivyo, uzalishaji katika shamba hilo ulisimama tangu mwaka 1995 na kubaki pori na huku wananchi wa kijiji hicho wakikosa maeneo ya kufanyia shughuli za kilimo, ufugaji na makazi.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Ngadinda, Kata ya Gumbilo, Halmashauri ya Madaba mkoani Ruvuma wakati wa ziara ya Waziri Mpina, wananchi hao walisema kwa miaka mingi wameishi kwa manyanyaso makubwa na hawajawahi kupata msaada wowote licha ya kufikisha kilio hicho serikalini.

Akizungumza wakati wa kutangaza uamuzi huo wa serikali, Waziri Mpina alisema baada ya wananchi kupaza sauti kulalamikia kukosa maeneo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mkoa wa Ruvuma, ilipima na kuweka mipaka inayoonekana na kubakiza hekta 4, 347 kwa ajili ya shughuli za mifugo za serikali.

Waziri huyo aliwataka wananchi wanaoishi katika vitalu namba mbili na 14 kuhama kwa hiari yao wenyewe ili kupisha shughuli za uzalishaji mifugo za serikali ziendelee chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuhudumia Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine nchini.

Pia, aliwataka wakulima wanaofanya shughuli za kilimo ndani ya eneo hilo lililobaki kwa ajili ya shamba la serikali, kusubiri kuvuna mazao yao na kuondoka na hawataruhusiwa tena

INAENDELEA UK. 8



Wanachi wakiangalia moja ya nyumba iliyopo kwenye jengo la ghorofa mali ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ikiteketea kwa moto, katika Kata ya Isamilo, jijini Mwanza juzi. Hakuna mtu yeyote aliyejeruhiwa, ila mali zote ziliteketea kwa moto. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Sababu mfumuko bei kubakia 3.8%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2019, umebaki kuwa asilimia 3.8 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba 2019.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minjah, alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Minjah alisema hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2019 imebaki kuwa sawa na kasi ya iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Novemba 2019.

Alifafanua kuwa mfumuko wa Desemba 2019 kubaki kuwa sawa kama ilivyokuwa Novemba 2019 umechangiwa na kuongezeka na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Desemba 2019, zikilinganishwa na bei za Desemba 2018.

"Kwa mfano baadhi ya bidhaa za vyakula zilizoongezeka bei kwa Desemba 2019, zikilinganishwa na bei za mwezi Desemba 2018 ni pamoja na mchele kwa asilimia 7.0, mtama kwa asilimia 3.3, nyama kwa asilmia 2.3, maharage kwa asilmia 7.7 na viazi mviringo kwa asilimia 2.7," alifafanua.

Aidha, alisema kwa upande mwingine baadhi ya bei za bidhaa zisizo za vyakula zilizopungua kwa Desemba 2019, zikilinganishwa na bei za mwezi Desemba 2018, ni pamoja na gesi ya kupikia kwa asilimia 2.1, mafuta ya taa kwa asilimia 7.1, jiko la kupikia la gesi kwa asilimia 1.6, mafuta ya petroli kwa asilimia 8.7 na dizeli kwa asilimia 8.7.

Pia alisema kuwa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Desemba 2019 umeongezeka hadi asilimia 6.3 kutoka asilimia 6.1 kwa mwaka ulioishia Novemba 2019.

Vilevile, alisema wastani wa mfumuko wa bei wa taifa kutoka mwezi Januari hadi Desemba 2019, umepungua hadi asilimia 3.4 mwaka 2019 kutoka asilimia 3.5 mwaka 2018.

"Wastani wa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula umeongezeka hadi asilimia 4.3 mwaka 2019 kutoka asilimia 3.7 mwaka 2018," alisema.

Alisema kwa upande mwingine wastani wa mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za vyakula kwa mwaka 2019 umepungua hadi asilimia 4.0 kutoka asilimia 4.3 ilivyokuwa mwaka 2018. "Wastani wa mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati umeongezeka hadi asilimia 3.0 mwaka 2019 kutoka asilimia 1.9 mwaka 2018," alisema.

Alisema baadhi ya bidhaa zilizochangia kuongezeka kwa wastani wa mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula kwa mwaka 2019 ni mavazi kwa asilimia 3.0 samani kwa asilimia 3.4, vyombo vya jikoni kwa asilimi 4.7 na gharama za kumuona daktari hospitali za binafsi kwa asilimi 4.1.

Kadhalika, vitabu vya shule kwa asilimia 2.2, madaftari kwa asilimia 2.0, ghara za ada kwa shule za msingi za binafsi kwa asilimia 2.5 na shule za sekondari za binafsi kwa asilimia 3.2.

Akizungumzia mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki, Minjah alisema Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2019 umeongezeka hadi asilimia 5.82 kutoka asilimia 5.56 kwa mwaka ulioishia Novemba 2019.

Kwa upande wa Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.0 kwa mwaka ulioishia Novemba 2019.

# Hospitali yapewa kibano dawa kwa wagonjwa

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amemwagiza Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Dk. Atupele Mwandiga, kuhakikisha anampatia taarifa ya utoaji wa dawa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa.

Agizo hilo limekuja baada ya ziara yake mkoani humo alipotembelea hospitali hiyo kujionea utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Katika ziara hospitalini hapo, Dk. Ndugulile, alisema amekasirishwa na utendaji kazi wa manesi katika wodi ya mama na mtoto kwa kutozingatia utoaji huduma hasa kuhakikisha wazazi na watoto wanapewa dawa kwa wakati zinazotakiwa na kwa idadi sahihi.

Alisema lengo la mgonjwa kupewa huduma ni kuhakikisha anapona na sio kusababisha aendelee kupata tabu, na kwamba hilo ndilo lengo kuu la serikali kuwekeza fedha nyingi katika sekta hiyo.

Dk. Ndugulile aliutaka uongozi wa Hospitali hiyo kuhakikisha wanaratibu utoaji wa huduma hospitalini hapo ili kuepukana na malalamiko ya wagonjwa na kupoteza imani ya wananchi kwa hospitali hiyo.

"Tukiendelea hivi tutaondoa imani kwa wananchi wetu katika utoaji wa huduma za afya, sisi tunatakiwa kutoa huduma kwa wananchi na sio kuwapa kero," alisema Dk. Ndugulile.

Dk. Mwandiga alimhakikishia Naibu Waziri kusimamia utoaji huduma bora katika hospitali hiyo.

# Wanusurika kifo ghorofa kuungua

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

FAMILIA sita zimenusurika kifo baada ya jengo la ghorofa mbili lililoko Mtaa wa Nyakabungo B, Nyamagana jijini Mwanza kuteketea kwa moto.

Jengo hilo linalomilikiwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) liliteketea juzi majira saa 12:00 jioni.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ambwene Mwakibete, alisema baada ya kupata taarifa walifika na kuuzima moto huo ambao ulikuwa tayari umeteketeza eneo la juu la jengo hilo.

Alisema sababu iliyowafanya kukwama kwa muda uokoaji ni kutokufika kwa wakati kwa wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hivyo akawataka wananchi kuendelea kutoa taarifa mapema pindi matukio kama hayo yanapotokea.

Naye Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi (ACP) Safia Jongo, alisema walipata taarifa ya tukio hilo na kuwaagiza askari waliokuwa lindo kufika eneo hilo kuimarisha ulinzi na kufanikiwa kuokoa mali za wakazi hao kwa kushirikiana na raia wema.

Pamoja na moto huo kuteketeza jengo hilo, Kamanda Jongo alisema hakuna vifo vilivyotokea.

Pia aliiomba jamii kutokutumia matukio kama hayo kuwa fursa ya kujinufaisha kwa kuwa watakuwa wanatenda matendo ya uhalifu yaliyokuwa kinyume cha sheria.

"Kuna vibaka walitaka kutumia hii nafasi vibaya kufanya uhalifu, lakini tuliwadhibiti vyema. Hakuna hata kijiko kilichoibwa," alisema Jongo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, alitoa pole kwa familia zilizopatwa na madhara na kuwataka kuwa watulivu wakati vyombo husika vikifanya uchunguzi wa kubaini chanzo cha moto huo.

Aidha, Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyakabungo B, Martine Michael, aliwataka viongozi wa Tanesco kuweka watu makini katika kitengo cha kupokea simu ili pindi matukio kama hayo yanapotokea wawe wepesi kupokea simu zinazotoa taarifa.

Samweli Petro na Sablina Zakaria, miongoni mwa wakazi wa eneo hilo, wakizungumza kwa masikitiko kuhusiana na tukio hilo, walisema waliona moshi na sauti za watu wakilia moto moto na walifika na kupiga simu Zimamoto ambao waliitikia wito muda huo.

"Cha kushangaza Zimamoto walipofika, walisimama kama dakika 15 pasipo kufanya chochote kwa sababu Tanesco walichelewa kufika ili kukata umeme eneo hilo, hivyo jengo liliendelea kuungua hadi pale walipokuja ndipo uzimaji ukaanza," alisema Petro.



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Augustino Mrema, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 7.**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Takukuru kuja kivingine teknolojia uchaguzi mkuu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Pwani, imesema vifaa vitakavyotumika mwaka huu kuwakamata wanaotoa na kupokea rushwa ni vya kisayansi, na havionekani kwa macho.

Hayo yameelezwa jana, Mjini Kibaha na Mkuu wa Kitengo cha Elimu kutoka Takukuru, Frendick Mbigili, wakati akitoa mada kwenye semina ya wenyeviti wa serikali za mitaa Kibaha Mjini iliyoandaliwa na Tanzania Development Forum (TADEFO).

Mbigili alisema, vifaa vitakavyotumika mwaka huu wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu kubaini rushwa ni vya kisayansi, hivyo hakuna mtu anayeweza kuona kwa macho. "Nyie wenyeviti ambao mpo madarakani kwa sasa tumeshirikiana sana wakati wa mchakato wa uchaguzi wenu, tunaamini tuko pamoja na nyie tunachowaomba ni kuendelea kuikataa rushwa katika majukumu yenu," alieleza na kuongeza:

"Vyombo vya kisayansi vitatumika kubaini rushwa kwa mwaka huu, havionekani kwa macho na hutamjua nani anacho kwenye kundi lenu, kinachotumika ni kuikataa rushwa na kutekeleza majukumu yenu kwa uadilifu."

Awali mmoja wa waalikwa katika semina hiyo Mchungaji Pascal Mnemwa, aliwatahadharisha wenyeviti kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa, kwani yamekuwa kero kwa jamii na kudumaza maendeleo.

"Hakuna imani inayosema rushwa inakubalika, viongozi wasiotimiza majukumu yao mara kwa mara wamekuwa wakitumia rushwa ili wananchi wawachague kwa kuwa hawana sifa za kuwa viongozi," alisema. Mnemwa alisema ni vema wenyeviti wa mitaa wakasimamia kikamilifu kwenye jamii yao na kuacha kutumiwa na wagombea ambao hawana sifa za kukubalika kuongoza na badala yake wamekuwa wakilazimisha kutoa rushwa ili wapate nafasi wanazotaka.

Naye Shekhe Hamis Mtupa alitoa wito kwa viongozi hao kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa hofu ya Mungu.

Wenyeviti hao walimpongeza Tadefo kwa semina hiyo ambayo imewakutanisha na kubadilishana uzoefu katika majukumu yao.

# Matukio 404 ukatili jinsia yaripotiwa Iringa

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

MKOA wa Iringa umekuwa na matukio takribani 404 ya vitendo ya ukatili wa kingono kwa watoto kati ya Januari na Novemba, mwaka jana.

Hayo yamebainika mkoani Iringa wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Afya, Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipotembelea vikundi vya malezi kwa watoto katika kijiji cha Kising'a kilichoko Wilaya ya Iringa. Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Iringa, Saida Mgeni, alisema mkoa wa Iringa unakabiliwa na matatizo mbalimbali na umekuwa ukiongoza katika masuala yasiyofaaa katika jamii, ikiwamo vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema serikali ya mkoa wa Iringa imejipanga katika kuhakikisha inapambana na vitendo hivyo dhidi ya wanawake na watoto kwa kuratibu utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya ukatili kwa wanawake na watoto.

Kutokana na maelezo hayo, Dk. Ndugulile alisema serikali haijalala wala kufumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto bali inachukua hatua kali dhidi ya wahusika wanaobainika.

Dk. Ndugulile alizitaka kamati za malezi ya mtoto mkoani Iringa na nchi nzima kuhakikisha wanatoa taarifa za vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kutowaficha watuhumiwa na hawamalizani kifamilia kesi za ukatili wa kijinsia. Aliongeza kuwa ni jambo la aibu kwa Tanzania ya viwanda kuwa na vitendo vya kikatili kutokea katika jamii kwa kuwa ni kikwazo kikubwa katika jamii kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

"Mkiona wanajamii miongoni mwenu wanataka kumalizana katika kesi za vitendo vya ukatili wa kijinsia, toeni taarifa ili tukomeshe vitendo hivi visiendelee nchini," alisema.

Dk. Ndugulile aliwataka wazazi na walezi nchini kuhakikisha wanakaa na kuzungumza na watoto wao badala ya kuwapiga na kuwapa adhabu zinatazosababisha kupata ukatili wa kisaikolojia ambao ni hatari kwa malezi na makuzi yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NEC iwape wananchi elimu endelevu kuongeza uelewa

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema moja ya changamoto zonazoikabili mara kwa mara ni jamii kushindwa kufahamu au kutofautisha kati ya uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa.

Hayo yalielezwa na Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mbarouk M'barouk, wakati akifungua mkutano wa NEC na wadau wa uchaguzi mkoani Lindi.

Jaji Mbarouk alisema yapo maeneo wananchi wake wamekuwa na mtizamo tofauti, wakifikiri uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi zote zinasimamiwa na tume hiyo, jambo ambalo sio la kweli.

Alisema uchaguzi wa serikali za mitaa unasimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wakati NEC inawajibika na usimamizi wa uchaguzi mkuu pekee, ambao unahusisha rais, wabunge na madiwani.

Alisema kwa kutotambua umuhimu wa jambo hilo, Tume imeamua kushirikisha wadau kushiriki katika michakato ya uchaguzi kwa lengo la kuwa karibu nao, ili kujenga imani kwa wananchi na kuweka uwazi wa utekelezaji wa majukumu yake.

Tume bila shaka imeone kuliweka wazi suala hili kwa kuwa ni kweli kwamba wananchi wengi wanashindwa kuelewa majukumu ya chombo hicho yanaishia wapi.

Kimsingi, wengi wanaendelea kuamini kuwa majukumu ya NEC ni kusimamia na kuratibu uchaguzi wote nchini; kwa maana uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa.

Pengine ndiyo maana makundi kadhaa katika jamii yamekuwa yakipendekeza kwamba uchaguzi wa ngazi zote wa kisiasa usimamiwe na NEC, kwa hoja kuwa ndicho chombo rasmi kinachowajibika kushughulikia masuala ya uchaguzi nchini.

Kutokuwapo kwa uelewa wa jamii juu ya majukumu ya NEC ni jambo linaloleta tafsiri kwamba utoaji wa elimu kwa umma kuhusiana na mchakato wa uchaguzi kwa ujumla, haujawa wa kutosha.

Kutokana na hali hiyo, changamoto inayoonekana ni kwa tume yenyewe kuchukua hatua za makusudi kwa kujikita zaidi katika utoaji wa elimu ya mpigakura kwa umma kuwa endelevu badala ya kusubiri uchaguzi unapokaribia.

Katika kuonyesha ukubwa wa tatizo la jamii yetu kuelewa kuhusu taasisi za kusimamia uchaguzi, mwaka jana wakati wa kuandikisha wapigakura kwenye daftari la wakazi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, kulikuwapo na mkanganyiko mkubwa.

Katika maeneo mengi wananchi walikuwa wakiamini kuwa kitambulisho cha mpigakura kinachotolewa na NEC ndicho kingetumika kupigia kura.


Mkanganyiko huo uliondoka baada ya Tamisemi kutoa matamko ya kusisitiza kuwa yenyewe ndiyo inayosimamia uchaguzi huo na kuweka wazi kuwa kitambulisho cha mpigakura hakitatumika, badala yake vitatumika vitambulisho vya aina saba.

Kwa kuwa NEC imeliona tatizo hili, tunaamini kuwa itachukua hatua haraka kulitafutia ufumbuzi, kupitia utoaji wa elimu endelevu, hivyo wapigakura kutambua majukumu ya NEC na ukomo wake.

Aidha, tunaishauri Tamisemi kutoa elimu kwa umma kuhusiana na jukumu na mamlaka yake ya kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa ili kuwaondolea wananchi mkanganyiko, na kuwawezesha kushiriki kwa wingi katika uchaguzi ujao.

Tunaamini kuwa elimu endelevu ndiyo inayoweza kuwapa uelewa wananchi katika masuala yote yanayohusu uchaguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Faini za kwenye taa maumivu makubwa

Na Salome Kitomari

**JUZI** katika safu hii, nilikuwa na hoja kuhusu hali inayojenga msuguano usio na msingi kati ya askari wa usalama barabarani na waendeshaji vyombo vya moto barabarani, jijini Dar es Salama. Leo pia, naendeleza hija yangu ndani ya jiji hilo.

Sehemu kuu ya hoja yangu ni namna fani zinazotozwa katika maeneo ya michoro ya wapitao kwa miguu, Zebra. Kwa kweli ujumbe mkuu ni kwamba, siridhiki nazo.

Niseme, katika makutano mengi ya barabara nyingi za Jiji la Dar es Salaam na mikoani, kuna taa za kuongoza magari, zinazowasaidia kuongoza magari kutembea kwa utaratibu maalum unaoiondoa mvurugano.

Taa hizo ni muhimu sana na inapotokea haziwaki kwa sababu mbalimbali na hakuna askari wa usalama barabarani, madereva hujikuta katika wakati mgumu sana, wakivuka mahali hapo kwa mtindo mwenye nguvu ndiye hupata nafasi.

Taa hizo na matumizi yake kisheria. Nyekundu inazuia magari kutembea, njano maana yake kaa tayari ama kuondoka au kusimama na rangi ya kijani, inaruhusu magari kutembea.

Kwenye baadhi ya mikoa kama Morogoro, taa zake zinaonyesha dakika, kwa hiyo dereva anaangalia dakika kabla ya kufanya uamuzi wa kupita au la, lakini kwenye maeneo mengine dereva, anapaswa kuangalia inapobadilika. Kwa Jiji la Dar es Salaam, taa hizo ni maumivu kwa madereva wengi kwa kuwa nyakati zote utakuta askari wamejificha hatua chache baada ya taa na wanavizia kila gari la mwisho, kupita kwenye taa hizo kwa ajili ya kutoza faini.

Kinachofanyika, ni kumvizia dereva ahukumiwe bila kusikilizwa, kwa kuwa moja kwa moja macho ya askari ndiyo yameona kosa na ndiyo yenye jukumu la kuamua dhidi ya dereva.

Mara nyingi unapokamatwa na trafiki cha kwanza atakwambia umepita kwenye taa nyekundu na unapaswa kumkabidhi leseni ili akutoze faini, na anayekwambia kosa na kutoa hukumu ya kukutoza faini ni askari mwenyewe. Makosa mengine kama ya kuzidisha mwendo huwa na ushahidi wa picha na kupunguza malalamiko kwa madereva, kwamba wanabambikwa makosa, lakini haya ya taa, hayana ushahidi wowote zaidi ya askari kuvizia gari ya mwisho na kuikamata.

Kwa sasa, askari wako kila mahali penye taa na wanavizia magari hasa kwenye maeneo yenye kona, Mathalani kwenye taa za makutano ya maktaba, vivyo hivyo katika Barabara ya Morogoro, makutano ya Chuo cha DIT, katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Eneo jingine ambalo wamewweka kibanda kabisa ni Salenda kuelekea Muhimbili, Oysterbay na barabara inayokatiza kuelekea Msasani, kote huko askari huwa katika mavizio kukamata gari ya mwisho.

Jambo hilo linatuogopesha sana madereva wengi kiasi kwamba unapofika kwenye taa, una gari dogo na la mbele yako ni gari kubwa, inakubidi usubiri liende umbali fulani ili uweze kuona taa ndipo upite.

Wakati mwingine unaondoka ulikokuwa umesubiri taa ikiwa kijani na ukiwa katikati au unamalizia unaona inawaka ya njano na hapo moja kwa moja askari huhesabu umekataa.

Pia, unapojaribu kujitetea, basi utaambiwa unamgomea askari na kinachofuata ni kupelekwa kituo cha polisi.

Madereva wengi kwa kuepuka usumbufu, wameandikiwa faini ambazo ni maumivu makubwa hasa kwa hali ya maisha ya leo, badala ya kuweka mafuta kwenye gari yako, unajikuta unalipa makosa ambayo ni ya kubambikiwa.

Ni vyema Jeshi la Polisi likafanya uchunguzi wa jambo hili kwamba faini za kwenye taa wanazotozwa madereva ni za haki au ni uonevu, japo nakiri wapo madereva kadhaa wasioheshimu taa hizo, hivyo kulazimishwa kutii sheria kupitia adhabu.

Nishauri, kwamba ni vyema Polisi wa Kitengo cha Usalama Barabarani, wakajadiliana na wanaoweka taa hizo na kuja na utaratibu kama unaotumika katika mikoa mingine, kwamba taa zihesabu dakika na dereva anapofika eneo hilo anaona kabisa ni dakika ngapi zimebakia kuliko, iliyopo sasa ya kubuni.

Naamini kabisa uwepo wa taa zenye kuhesabu dakika, utasaidia kupunguza malalamiko ya madereva na kuwasaidia askari kuondokana na lawama au watu kuwa na kinyongo kuwa faini wanazotozwa ni za uonevu.

Hakuna ubishi kwamba, pasipo utii wa sheria bila shuruti, hakuna barabara wala usafiri salama. Kila mtumiaji wa barabara, anapaswa kuheshimu sheria na kanuni za barabarani, kuliko kufanya anavyotaka.

Wasimamizi wa sheria hizo, nao wanapaswa kuhakikisha wanatenda haki inayoonekana imetendeka, kuliko kuonea au kutoa adhabu zisizostahili kwa madereva na ikifikia hatua ya kuwepo taa zenye kuhesabu dakika, kutasaidia sana.

## EPZA yatoa gawio kwa serikali mil. 100/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) imetoa mchango wa Sh. milioni 100 katika kuunga juhudi za serikali kuongeza mapato ya ndani ili kutekeleza ajenda ya maendeleo. Akizungumza baada ya kupokea gawio na michango kutoka kwa taasisi mbalimbali jana jijini Dodoma, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alizishukuru taasisi hizo kwa kutii agizo la Rais John Magufuli la kuzitaka taasisi zote kulipa gawio na michango kabla ya mwisho wa mwezi huu.

"Kwa namna ya pekee nazishukuru taasisi hizi kwa kutoa gawio na michango hii ambayo ni muhimu sana katika kuisaidia serikali kuboresha maisha ya wananchi wake," alisema.

EPZA inaungana na taasisi nyingine takribani 266 kutoa mchango kwa serikali ili kuboresha makusanyo na mapato ambayo ni muhimu katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katika tukio la jana lililofanyika jijini Dodoma na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali, EPZA iliungana na taasisi nyingine 12 katika kutoa michango na gawio kwa serikali.

Dk. Mpango alisema mapato ya ndani yanapoongezeka kutoka vyanzo mbalimbali huisaidia serikali kupunguza mikopo ya nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa taasisi mbalimbali za serikali zimetoa gawio na michango yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni moja katika mwaka fedha wa 2018//19 ikiwa imeongezeka kutoka Sh. bilioni 161.04 mwaka 2014/15 uliotolewa na taasisi 24 pekee.

Mamlaka ya EPZA iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ina wajibu wa kutekeleza sera ya serikali ya kuhamasisha na kuvutia uwekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi ya EPZ nchini.

Meneja wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, Grace Lemunge, alisema mamlaka inatoa huduma nyingi kuvutia uwekezaji katika viwanda ikiwa ni pamoja na kutoa leseni, uhamasishaji, uwekezaji na kuendeleza miundombinu katika maeneo maalumu ya kiuchumi.

"Maeneo maalum ya EPZ huvutia uwekezaji wa viwanda ambavyo huzalisha bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi wakati maeneo ya SEZ huvutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na nje," alisema.

# Mrema amwandikia JPM

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Augustino Mrema, amemwandikia barua Rais John Magufuli, akiomba kulipwa fidia ya Sh. bilioni mbili kwa kile alichodai Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumfanya kuwa dhaifu kisiasa.

Amedai serikali ya chama hicho kwa muda mrefu imefanya mambo mbalimbali kuhakikisha inammaliza kisiasa, akieleza kuwa moja ya mikakati hiyo ni kufungulia kesi mahakamani tangu mwaka 1995.

"Tangu mwaka 1995, serikali na CCM imekuwa ikinitafuta kunidhoofisha kisiasa, nimeandika barua kwa Mheshimiwa Rais tupewe fidia ya Sh. bilioni mbili. Naomba Rais wa awamu ya tano afute kabisa hiyo historia," aliomba.

Mrema alizitaja kesi alizofunguliwa na serikali kuwa ni pamoja na kesi namba mbili ya mwaka 1997 aliyodaiwa kumuhusisha Rais wa awamu ya tatu, Benjamini Mkapa, na rushwa ya Sh. milioni 500.

Alikumbusha jinsi alivyokamatwa na kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kujibu mashtaka yaliyokuwa yanamkabili kuhusu kesi hiyo, akidai ilikuwa sehemu za njama za kummaliza kisiasa.

INAENDELEA UK. 8

TANZANIA ZAMBIA RAILWAY AUTHORITY

## KURUDISHWA KAZINI

Kufuatia oda ya Mahakama Kuu Kitengo cha Kazi, shauri namba CMA/DSM/ILALA/R.965/17 inayoitaka TAZARA kuwarudisha kazini wafanyakazi 35 walioachishwa kazi , Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia inawatangazia wafanyakazi hao wafike mara moja kwenye vituo vyao vya awali vya kazi, kwenye ofisi ya Rasilimali watu ili waweze kuchukua barua zao za kurudi kazini kama ilivyoelekezwa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya tangazo hili.

**Majina yao ni kama ifuatavyo.**

| S/N | NAME | DESIGNATION | STATION |
|---|---|---|---|
| 1 | Anna Fabian | Typist | DSM |
| 2 | Said Ndee | Shunter | Yombo |
| 3 | Frank Lubilo | Artisan | DSM |
| 4 | Mwanahamisi Juma Shunda | Artisan | DSM/WSHOPS |
| 5 | Ivod Mosses Gwalasa | Artisan | Mbeya |
| 6 | Alex L Kayage | Artisan | Yombo |
| 7 | Hilda Mtaya | Pointsman | Mbalizi |
| 8 | Rahel Myombe | Pointsman | Mbeya |
| 9 | Victor S. Revo | Pointsman | Yombo |
| 10 | Godfrey Jackson Mwangoka | Artisan | DSMW/SHOPS |
| 11 | Adriano F. Katene | Artisan | DSM W/SHOPS |
| 12 | Azizi S. Mkuya | Artisan | DSM W/SHOPS |
| 13 | Ibrahim Adam | Artisan | DSM W/SHOPS |
| 14 | Said A. Mdemu | Pointsman | Mbalizi |
| 15 | Simon M Marwa | Trainguard | Mlimba |
| 16 | Peter Titus Machaku | Leading Artisan | DSM |
| 17 | Dawama Ally Ismail | Artisan | MBYW/shop |
| 18 | Sued Semgaya | Number Teker | DSM |
| 19 | Deogratias Deus Rutter | Trainexaminer | Yombo |
| 20 | SADOCK NTOLE | Mechanical Fitter | Mbeya |
| 21 | HAJI S HIMBUKA | Motor Vehicle Driver | Dar es Salaam |
| 22 | BENSON KYELUSYA | Station Foreman | Dar es Salaam |
| 23 | SHABANI MGWENO | Leading Artisan | Dar es Salaam |
| 24 | CYPRIAN CHIFWILA | Artisan (Painting) | Dar es salaam |
| 25 | JOHN TIRA | Artisan (B/Smith) | Mbeya |
| 26 | CHRISTOPHER MASASI | Station Foreman | Yombo |
| 27 | LUCAS S NTILA | Station Foreman | Mlowo |
| 28 | JULIUS B MUKAMA | Locomotive Driver | Yombo |
| 29 | HAMIS A OBHUNGA | Artisan(W&P) | Mbeya |
| 30 | SAMORA A MBWELWA | Artisan (Fitter C&W) | Dar Es Salaam |
| 31 | SEIF K KIYANGA | Train Guard | Mbeya |
| 32 | DANIEL Y MWAIKUSA | Artisan (Carpenrty) | Dar Es Salaam |
| 33 | BARTON KIGOLA | Artisan (C&W) | Dar Es Salaam |
| 34 | TUNGAI E MESHACK | Water Pump Attendar | Ifakara |
| 35 | MWARAMI A MOHAMEDI | Train Examiner(C&W) | Mlimba |
| | TOTAL | | |

**Imetolewa na Meneja Mkuu,**
**TAZARA Tanzania**

# Mrema amwandikia JPM

INATOKA UK. 7

Mrema alidai kuwa hata baada ya kushinda kesi hiyo, iliundwa Kamati ya Bunge ili kuchunguza nyaraka zilizokuwa zikihusisha tuhuma za rushwa dhidi ya vigogo mbalimbali wa serikali ya CCM.

"Hata hivyo, kamati haikunipata na hatia na ilinipatia cheti cha kinga ya kutoshtakiwa ndani ya kamati hiyo ya Bunge," Mrema alitamba.

Hata hivyo, Mrema alidai kuwa mwaka 1999 alifunguliwa kesi nyingine namba 61 ya mwaka huo, muda mfupi baada ya kushinda ubunge wa Jimbo la Temeke, akidaiwa kutoa ushahidi wa uongo mbele ya Kamati ya Bunge licha ya awali kupewa kinga ya kutoshtakiwa na Kamati ya Bunge.

"Mheshimiwa Rais, fitina hizo zilifanya wajumbe kuneemeka kwa kujaribu kuniangamiza kisiasa kwani kamati iliyoundwa kwa ajili yangu, wote walipewa vyeo," Mrema alidai wakati akisoma mbele ya waandishi wa habari barua yake aliyomwandikia Rais Magufuli. Alidai kuwa harakati hizo ndizo zilizosababisha kuyumba kwake kisiasa na kukosa wafuasi na kusisitiza kuwa matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana yamemkumbusha machungu yote aliyopitia katika safari yake ya kisiasa tangu mwaka 1995 na kufikia uamuzi wa kuandika barua kudai fidia hiyo.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa sasa sina hata mtaa mmoja unaoongozwa na TLP na hata kule kijijini kwangu Kiraracha, ambako ikitokea nikifa, watu wangu watanizika, huko wamenipora, nilienda nikakuta magari ya polisi akiwamo na Mkuu wa Mkoa, wote wako huko kuhakikisha wananipora viongozi wangu," Mrema alidai.

Kiongozi huyo wa kisiasa, alidai kuwa licha ya urafiki na ushirikiano alionao kwa serikali ya Rais Magufuli, alishangazwa na nguvu kubwa iliyotumika katika uchaguzi huo, aliodai mawakala wake waliondolewa kwa nguvu na Jeshi la Polisi na kusababisha chama chake kukosa mawakala katika uchaguzi huo.

**MREMA NI NANI?**

Mrema (75), aliwahi kuwa mwanachama wa CCM, alikotumika kama mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani. Pia aliwahi kuwa mwanachama wa NCCR Mageuzi, alikowania urais na kuwa miongoni mwa wagombea watatu waliofanya vizuri katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995.



Wanafunzi wa darasa la awali na msingi wa Shule ya Msingi Agape, kijiji cha Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara wakisubiri kushuhudia uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la Tehama la shule hiyo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpina atatua mgogoro uliodumu kwa miaka 10

INATOKA UK. 4

kufanya shughuli zozote za kilimo kwenye shamba la mifugo au eneo la pembezoni mwa shamba hilo.

Vilevile, wafugaji waliopo katika vitalu ambavyo kwa sasa vitakuwa ni eneo la wananchi, wanatakiwa kupisha eneo hilo litumike kwa ajili ya makazi na kilimo.

Mpina alisema wafugaji walioko vitalu vyote vilivyoko katika shamba hilo, watatakiwa kuhamia katika eneo la shamba lililopo Mhukulu Lilahi baada ya taratibu za kutenga vitalu katika shamba hilo kukamilika.

Waziri huyo aliitaka Halmashauri ya Madaba kugawa eneo hilo kwa wananchi kwa malengo yaliyokusudiwa, huku akiwataka wananchi wa eneo hilo kuwa watulivu na kuheshimu mipaka iliyowekwa na kutoingia tena kwenye shamba la serikali lililobaki kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa mifugo ili kusitokee tena mgogoro baina ya wananchi na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alimshukuru Waziri Mpina kwa kumaliza mgogoro uliowashinda viongozi mbalimbali na kumshukuru Rais John Magufuli kwa kuwa na aina hiyo ya mawaziri wanaochambua kwa makini matatizo ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu.

Mbunge wa Madaba, Joseph Mhagama, alisema mgogoro huo ulikuwa ukiwakosesha usingizi wananchi kwa kuwa wamekuwa wakikamatwa na kupelekwa mahakamani.

Mhagama alimshukuru Waziri Mpina kwa kuwa kiongozi mnyenyekevu na anayegusa na matatizo ya wananchi na kuamua kukubali kumega hekta 1,800 kuwagawia wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo na makazi.

# Matatani kwa tuhuma za kumteka raia wa Marekani

INATOKA UK. 3

walilokuwa wamempakia.

Alisema licha ya watuhumiwa hao kukimbia, walifanikiwa kumwibia Brandjester Sh. 500,000 na fedha nyingine za kigeni.

Alisema kuwa mtuhumiwa huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi, na baadaye hatua za kisheria zitafuata.

Brandjester amekuwa Zanzibar tangu Desemba 30, mwaka jana, na alifikia Kijiji cha Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Jeshi la Polisi lilieleza zaidi kuwa watuhumiwa hao walijifanya ni raia wa Somalia, na kumtishia kuwa wana kisasi na Wamarekani.

Kamishna wa Polisi Zanzibar, Mohammed Hassan, alisema kuwa jeshi hilo linaendeleza jitihada za kupambana na uhalifu na kuongeza kasi ya doria katika maeneo ya utalii kudhibiti uhalifu.

Alieleza kuwa uhalifu visiwani Zanzibar umepungua kwa kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2019, ambapo matukio makubwa ya jinai 2,911 yaliripotiwa ukilinganisha na matukio 2,531 yaliotokea mwaka 2018.

Alieleza kuwa kati ya matukio hayo yaliyoripotiwa mwaka 2019, makosa dhidi ya binadamu yalikuwa 975, makosa ya kuwania mali ni 1,467 na makosa dhidi ya maadili ya jamii ni 89.

## Waziri: Vigogo taasisi 36 wasiende ofisini Jan 24

INATOKA UK. 2

yamepanda kutoka Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi hadi trilioni 1.75, akitamba kuwa sasa hakuna wa "kutusumbua sumbua".

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema katika eneo ambalo walilisahau ni hilo la kutoa gawio ilhali serikali imekuwa ikiwekeza fedha nyingi.

"Tumeona Rais na mwelekeo wake wa kusimamia rasilimali za taifa letu, hivyo awamu ya tano imekuwa mfano bora katika kutekeleza jambo hilo.

"Gawio kwa vyuo vikuu haikuwahi kutokea, lakini kupitia Rais wa awamu ya tano imewezekana, hivyo Watanzania tukiamua jambo kwa pamoja, tunaweza kwani kuna ongezeko la zaidi ya asilimia 552, hivyo tunaiambia dunia kuwa tuko vizuri," alisifu.

Msajili wa Hazina, Athuman Mbutuka, alizitaja taasisi 13 zilitoa gawio kwa serikali jana kuwa ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Star Media, Wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA), Procument & Supplies Proffessional Technian Board, Bodi ya Utalii (TTB), NDC, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU), Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU), Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (Muhas), Export Processing Zone Authority (EPZA), Agriculture Input Trust Fund na Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT).

## Mwanamke asimulia kortini alivyobakwa na mkimbizi

INATOKA UK. 3

alichokifanya.

Shahidi huyo alidai mahakamani kuwa mshtakiwa aliomba msamaha na kusema asimpeleke kwenye kituo cha IRC kwa madai kuwa atampa fedha nyingi maana akimpeleka huko watamfunga lakini alikataa na kudai kuwa mshtakiwa huyo anaweza kuwa na virusi vya Ukimwi, hivyo ni lazima akapime kwenye zahanati ya IRC.

Aliendelea kudai kuwa alipofika kwenye Zahanati ya IRC alimkuta mama mmoja akamsimulia kilichotokea ndipo alimpa msaada wa kumpeleka kituo kikuu cha polisi na kupewa PF3 kisha kwenda Hospitali ya Rufani ya Maweni.

Shahidi alidai kuwa alipofika hospitalini hapo, alifanyiwa uchunguzi kisha kupewa dawa na barua ya kupeleka kituo kikuu cha polisi na kurudi kwenye kambi ya NMC iliyoko Kibirizi Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 16, mwaka huu, kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliyobaki na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu katika Gereza la Bangwe hadi hapo atakapopata wadhamini.

Hakimu Mwakitalu aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni moja.

# Hatarini kukumbwa magonjwa ya mlipuko

**Na Jumbe Ismailly,** ITIGI

WAKAZI wa Kijiji cha Rungwa, Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni, wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya kuambukiza, ikiwamo kuhara damu kutokana na kunywa maji yanayopatikana kwenye vidimbwi yasiyo safi na wala salama.

Mmoja wa wakazi hao, Raheli Nira, alisema jana kuwa pamoja na kuwapo mradi wa kisima cha maji walichochimbiwa na Kampuni ya Majitech, wamelazimika kuendelea kunywa maji yanayopatikana kwenye madimbwi ya mvua kutokana na yale ya mradi wao wa kijiji kuwa na chumvi.

"Sisi tuna kero ya maji kijijini kwetu. Maji yamepatikana lakini maji haya ni ya chumvi, hivyo bado hayakidhi mahitaji ya Kijiji cha Rungwa," alisema Nira.

Kwa mujibu wa mkazi huyo, wanamwomba mkandarasi aliyekuwa akijenga bwawa la Rungwa, aliyetoweka katika mazingira ya kutatanisha, arudi haraka kwenye eneo lake la mradi kumalizia kazi iliyobaki ili wanufaike na maji hayo ambayo hayana chumvi.

"Wananchi tunatumia maji ya kwenye madimbwi yasiyokuwa salama yanayouzwa kwa Sh. 500 kwa dumu moja lenye ujazo wa lita 20. Tunaiomba serikali isituacahe watu wa Rungwa, mkandarasi aje akamilishe kazi aliyokabidhiwa," alisema. Mkazi huyo alisisitiza kwamba maji wanayokunywa ni machafu kwa sababu yanachotwa kwenye mabwawa na pia hayakidhi mahitaji ya wakazi wa Kijiji cha Rungwa na vitongoji vyake.

Naye Serafina Mlowosha, Mwenyekiti wa Watumiaji Maji Kijiji cha Rungwa, alisema licha ya maji ya kisima kilichochimbwa na kampuni ya Majitech kuwa na chumvi, ndiyo ambayo yamewakomboa baada ya maji ya bwawa la Rungwa kukatika.

"Nafikiri huwa tunatumia kama jinsi tulivyokuwa tumepewa ushauri yale maji yanatakiwa yatibiwe. Baada ya kujazwa kwenye tangi yanatibiwa, mtu anaruhusiwa kunywa vinginevyo tunachemsha maji tunakunywa." Alisema.

# Waziri aagiza kutumbuliwa kigogo ardhi

**Na Munir Shemweta,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kuondolewa katika nafasi Mkuu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, Mariam Kimoro.

Hatua hiyo imetokana na Naibu Waziri kutoridhishwa na utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika halmashauri hiyo.

Dk. Mabula alisema mkuu huyo wa idara ameshindwa kusimamia vyema ukamilishaji wa hati za ardhi 150 zilizoombwa na wamiliki wake kwa miaka tofauti kuanzia mwaka 2011.

Akizungumza juzi wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani Mtwara, Dk. Mabula alisema haiwezekani hati za ardhi kuandaliwa tangu mwaka 2011 na hadi sasa wamiliki wake wameshindwa kutia saini kwa ajili ya kumilikishwa jambo alilolieleza linaikosesha pia serikali mapato.

"Hatuwezi kuwa na mkuu wa idara asiyefanya kazi ipasavyo, anasubiri watu waje watie saini na hakuna jitihada zozote zilizofanyika kuwatafuta mmiliki na hata kuwapigia simu?" Alisema Mabula.

Ofisa Ardhi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani, Edna Chacha, aliitetea idara hiyo kwa kueleza kuwa imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kukamilisha hati za ardhi lakini changamoto kubwa ni wamiliki kushindwa kujitokeza.

Naibu Waziri Mabula alipingana na ofisa huyo kwa kumweleza kuwa haiwezekani wamiliki 150 kwa pamoja washindwe kupatikana kwa ajili ya kutia saini ili wamilikishwe na kubainisha kuwa hali hiyo inachangiwa na uzembe wa idara hiyo kushindwa kuwafuatilia wamiliki hao.

Dk. Mabula ambaye alitembelea pia halmashauri za Mtwara na Nanyamba, alizitaka idara za ardhi kwenye halmashauri za mkoa wa Mtwara kujipanga katika kushughulikia masuala ya ardhi, ikiwamo kuingiza majalada ya ardhi kwenye mfumo wa kielektroniki kwa asilimia 100.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri alielezea kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini iliyopo eneo la Mitengo mkoani Mtwara.

Ujenzo huo unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu na kugharimu takribani Sh. bilioni 15.8, unafanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na utahudumia mikoa ya Mtwara, Songea, Lindi na nchi jirani ya Msumbiji.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa jengo hilo, Dk. Mabula aliipongeza NHC kwa kujenga jengo hilo kwa kasi aliyoieleza kuwa italifanya jengo kukamilika kabla ya muda uliopangwa.

Meneja wa NHC Mkoa wa Mtwara, Angelina Magazi, alisema shirika limejipanga kuhakikisha ujenzi huo unakamilika mapema na kubainisha kuwa kwa sasa unafanyika usiku na mchana.




Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mwanza, Albogast Kajungu, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu kituo cha upimaji uwezo wa matangi ya magari ya kubebea mafuta, kilichopo Nyamongoro, jijini humo kinavyofanya kazi. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Hakimu akwamisha kesi m/kiti halmashauri

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

KESI inayomkabili Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Peter Maloda, ya kuingia kwa jinai kwa kuvamia shamba la Tungu Ntegwa, imeshindwa kuendelea kusikilizwa.

Kesi hiyo iliyoko katika Mahakama ya Mwanzo ya Choma, ilishindwa kusikilizwa kutokana na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Ziba, Goodluck Pallangyo, kutofika mahakamani hapo.

Hakimu Pallangyo amepangiwa kusikiliza kesi hiyo baada ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Choma, Simon Malima, kujitoa kwa hofu ya kutotenda haki kwa kuwa mmoja wa washtakiwa ni jirani yake. Katika maelezo ya shtaka hilo, inadaiwa kwamba Desemba 16, mwaka jana, saa 3:00 asubuhi, Maloda na Ndekwa Usukani, walikutwa wakilima shamba la mlalamikaji Ntegwa, mkazi wa Kijiji cha Choma bila idhini yake, huku wakijua kuwa kufanya hivyo ni kosa na kinyume cha sheria.

Washtakiwa hao baada ya kusomewa shtaka, walikana na kwamba wote wako nje kwa dhamana ya Sh. 500,000 kila mmoja na mdhamini mmoja.

Akiahirisha kesi hiyo ambayo ilikuwa ianze kusikilizwa kwa mara ya kwanza, Hakimu Malima alisema kuwa Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Igunga, ameihamishia kesi hiyo katika Mahakama ya Mwanzo ya Ziba na kwamba itaendelea kusikilizwa na hakimu wa mahakama hiyo.

Baada ya mahakama kutoa uamuzi huo, ndipo mlalamikaji katika shauri hilo alidai kuwa hana uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 50 kwenda na kurudi iliko mahakama hiyo, hivyo kuiomba Mahakama ya Wilaya kuirudisha kesi hiyo Choma.

Aidha, Ntegwa aliiomba pia mahakama hiyo itoe amri ya kusitishwa matumizi ya shamba hilo hadi hapo kesi hiyo itakapomalizika kusikilizwa na kutolewa uamuzi. Kutokana na madai hayo,

Hakimu Malima alimshauri mlalamikaji kupeleka maombi yake kwa maandishi kwa Hakimu wa Wilaya ya Igunga kuhusu kesi hiyo kurudishwa Choma.

Kuhusu amri ya kusitisha matumizi ya shamba, hakimu alimtaka mlalamikaji huyo kupeleka ombi hilo kwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Ziba kwa uamuzi zaidi.

# Watumishi wapewa somo utendaji kazi

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

WATUMISHI wa umma wametakiwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kufanikisha juhudi za Rais John Magufuli za kukuza uchumi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika ziara ya kikazi mkoani hapa.

Mwanjelwa alisema ni lazima watumishi wa umma waheshimu kazi na wahakikishe wanatimiza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo kwa kuwa serikali haitawavumilia watumishi wazembe.

"Mtumishi wa umma ni tunu kwa hiyo ni bora ukachezea mshahara kuliko kuchezea kazi kwa sababu wapo wanaotamani kuingia serikalini, lakini hawana fursa hiyo," alisema.

Mwanjelwa alitoa wito kwa watumishi wa umma nchini kufanya kazi kwa kuendana na spidi ya Rais Magufuli na si kwa kulegalega na kuongeza kuwa serikali ni ya uadilifu, utendaji kazi uliotukuka, haki na haiko tayari kumwonea mtumishi yeyote.

Pia aliwataka watumishi wa umma kuwa na subira katika kipindi ambacho serikali inafanyia kazi malimbikizo ya mishahara, kupandishwa madaraja na mambo mengineyo.

Mwanjelwa yuko katika ziara ya kikazi mkoani Singida kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) na kukutana na watumishi kwa lengo la kusikiliza maoni na kutatua kero zao.

## Vifo vya mifugo sasa kupungua

**Na Gurian Adolf,** NKASI

SERIKALI imeanzisha kampeni maalumu ya kupambana na magonjwa ya mifugo kwa kusambaza dawa katika majosho yote ikiwa ni jitihada za kuwasaidia wafugaji kuondokana na changamoto ya mifugo kufa.

Ofisa Mifugo Mfawidhi wa Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo Kanda ya Kusini Magharibi, Dk. Kaini Kamwela, alisema juzi kuwa huo mkakati wa serikali katika kuhakikisha wafugaji wanafuga mifugo kitaalamu.


Alisema kwa muda mrefu wafugaji wamekuwa wakikumbana na changamoto ya kushindwa kuogesha mifugo kutokana na ukosefu wa dawa pamoja na gharama ya kuogeshea mifugo kuwa kubwa.

Alisema kwa kutambua hilo serikali imepunguza gharama za kuogeshea mifugo kwa asilimia mia moja.

Aliyasema hayo baada ya kutembelea josho la kuogeshea mifugo lililoko katika Kijiji cha Kate, Nkasi mkoani Rukwa.

Baadhi ya wafugaji katika kijiji hicho, waliipongeza serikali kwa jitihada hizo na kusema awali walikuwa wakiogesha mifugo kwa bei kubwa, hivyo kusababisha kushindwa kumudu gharama sambamba na matibabu kuwa juu.

"Tunaishukuru sana serikali kwa jitihada zake katika kutupatia dawa za mifugo pamoja na kuongeza idadi ya mashojo. Hatua hiyo itatuwezesha kuondokana na changamoto ya kufa kwa mifugo yetu," alisema Jilala Nkwabi mmoja wa wafugaji katika kijiji hicho.




Kaimu Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 20, kwa mkazi wa Ilala, Hajira Fadhil, baada ya kuibuka mshindi wa kitaifa wa kampeni ya Tigo Pesa Wakala Kinara, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wakulima korosho wapigiwa debe NHIF

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WAKULIMA wa korosho mkoani Mtwara, wamehimizwa kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kujihakikisha upatikanaji wa matibabu ya afya.

Ushauri huo ulitolewa jana mkoani hapa na Meneja wa NHIF Mkoa wa Mtwara, Silvery Mgonza, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma za mfuko huo.

Alisema ni vyema wakulima wa korosho katika mkoa wa Mtwara wakafahamu umuhimu wa kujiunga na mfuko huo ili kujihakikishia upatikanaji wa matibabu.

Mgonza alisema wakulima wa korosho kupitia ushirika wao, wanaweza kujiunga kwa umoja wao katika mfuko huo na hatimaye kuwa na fursa ya kuwa wanachama.

Kwa mujibu wa meneja huyo, azma ya NHIF ni kuhakikisha wakulima wote wanakuwa wanachama wa mfuko huo kwa kujiunga wakati huu wa msimu wa korosho.

Alisema msimu wa korosho bado unaendelea, hivyo ni wazi kuwa wakulima wanalipwa fedha zao jambo ambalo ni rahisi kwao kuhamasishana kupitia ushirika walio nao na kujiunga kwenye mfuko huo.

NHIF, alisema bado inaendelea kuhamasisha jamii mzima ili kufahamu umuhimu wa kujiunga na kufurahia vifurushi vya mfuko huo katika kupata mahitaji ya msingi.

"Tunataka wakulima wa korosho wahamasike na wawe na utayari wa kujiunga na bima ya afya ili iwe rahisi kwao kupata matibabu," alisema Mgonza.

Alisema umoja au ushirika wa wakulima ni mkubwa, hivyo kwa umoja wao wakijiunga na mfuko, itasaidia suala la huduma za kiafya kwa unafuu zaidi.

Mgonza alitumia fursa hiyo kuwahimiza wakulima wa korosho katika mkoa wa Mtwara kujiunga na mfuko huo kwa ajili ya urahisishaji wa kupatikanaji wa matibabu.

Musa Abdallah, mkulima wa korosho mkoani Mtwara alisema mpango huo wa bima ya afya iwapo wakulima wakiutumia vyema na kujiunga, utawasaidia katika kupunguza gharama za matibabu.

# DC aagiza wazazi kupeleka chakula shuleni

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, amewataka wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuwapelekea watoto wao vyakula vya mchana, ili kuepusha usumbufu wa kwenda na kurudi nyakati hizo.

Chaula, alitoa agizo juzi wakati akizungumzia jukumu la upatikanaji wa vyakula kwa wanafunzi wa shule zilizopo wilayani humo.

Alisema kutokana na jiografia ya umbali mrefu kati ya shule ni vyema wazazi wakaweka utaratibu wa kuhakikisha chakula kinawafikia watoto wao shuleni badala ya kurudi nyumbani kula chakula cha mchana.

Aidha, kutokana na umbali huo ameshaagiza wazazi na walezi kuchangia chakula ili watoto wao wale chakula shuleni, ambayo itasaidia kuongeza kiwango cha taaluma shuleni.

"Walimu hawapaswi kushika fedha au kuwa kwenye kamati za fedha za chakula, kuna mwongozo wa serikali unatamka hilo, ila wazazi na walezi pekee ndiyo wenye jukumu la kusimamia," alisema Chaula.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema tangu kufunguliwa kwa shule wanafunzi 4,496 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza.

Myenzi alisema shughuli ya uandikishaji inafanyika kwa muda muda wa miezi mitatu na kwamba inaendelea.

Kadhalika, alisema Wilaya ya Simanjiro haina tatizo la upungufu wa madarasa ya watoto kusomea, hivyo kazi inayofanyika kwa sasa ni kukagua na kuratibu zoezi la uandikishaji wa wanafunzi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mirerani, Tenisia Elias, akizungumza na wazazi na walezi waliowapeleka watoto shuleni hapo, alisema wanapaswa kuandikisha majina ya watoto wao kwa mtendaji wa vitongoji.

Elias alisema wazazi na walezi wanatakiwa kuandikisha majina ya wanafunzi kwa watendaji wa vitongoji na baada ya uandikishaji viongozi hao watayafikisha majina hayo shuleni.

"Pamoja na hayo wazazi na walezi huwa mkienda kwenye mikutano ya vitongoji na vijiji mnatangaziwa kuchangia vyakula ili watoto wale shuleni, lakini leo sioni hata mzazi aliyebeba chakula," alisema.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, akimwonyesha mkandarasi wa kampuni ya Beijing Construction Engineering Group, Liang Li, ramani ya jengo la makao makuu ya mashirika ya Posta Afrika, litakalokuwa na ghorofa 16, baada ya kumkabidhi eneo litakapojengwa jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mbulu, Simanjiro zaandikisha wanafunzi 11,296 la kwanza

**Na Allan Isack,** MBULU

JUMLA ya watoto 11,296 wa wilaya za Mbulu na Simanjiro mkoani Manyara, wameandikishwa kujiunga na darasa la kwanza kwa mwaka 2020.

Imeelezwa kuwa Wilaya ya Mbulu watoto 6,885 wameandikishwa kujiunga na shule ya awali. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Hudson Kamoga, akizungumza na Nipashe alisema idadi hiyo inaonyesha mwitikio mkubwa wa wazazi kuwaandikisha watoto wao kuanza elimu ya msingi.

"Kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi ni 3,099 tunatarajia wote watajiunga kidato cha kwanza mwaka 2020, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu," alisema Kamoga.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, shule za sekondari hakuna upungufu wa vyumba vya madarasa, lakini baadhi ya shule za msingi kuna tatizo hilo.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, serikali imetoa fedha za kumalizia baadhi ya vyumba vya madarasa ya shule za msingi, baada ya wazazi kujenga na kufikisha kwenye hatua ya maboma.

Kwa upande wake Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu Msingi wilayani Simanjiro, Abdalah Hamis, alisema hadi hivi sasa wanafunzi 4,496 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2020.

Hamis alisema kati ya wanafunzi hao, wavulana ni 2,466 na wasichana ni 2,050 na wanaendelea kuandikisha hadi mwezi Machi mwaka huu.

Aidha, alisema kwa upande wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi wilayani humo, mahitaji ni 964, na yaliyopo ni 577 na pungufu ni 387.

Alifafanua kuwa matundu ya vyoo mahitaji yake ni 1,768 yaliyopo ni 1,008 na pungufu ni 760. "Madawati yanayohitajika ni 14,103 yaliyopo ni 12,068 na pungufu ni 2,094 kwenye Wilaya ya Simanjiro," alisema.

# Kamwele akabidhi eneo ujenzi Papu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwele, jana, amekabidhi eneo la ujenzi wa jengo la makao makuu ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) lililopo mjini Arusha, kwa mkandarasi wa kampuni ya Beijing Construction Engineer.

Akizungumza jana, jijini Arusha, baada ya kukabidhi eneo hilo kwa mkandarasi huyo, ambaye ni Meneja wa kampuni hiyo, Li Liang, Mhandisi Kamwele aliagiza jengo hilo la ghorofa 16 la thamani ya Sh. bilioni 30 likamilike ndani ya miezi 30 iliyopangwa.

"Lakini ikibidi likamilike kabla ya muda uliopangwa na hapa eneo la ujenzi hakuna kuingia mtu yoyote ni wale tu wenye kibali cha Wizara ya Mambo ya Nje, kwani ni eneo la Umoja wa Mataifa hapa," alisema.

Alisema lazima paheshimiwe hapo kuanzia jana Januari 8, alipokabidhi tayari kuanza kwa ujenzi huo na hata baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

Aidha, alisema jengo hilo linajengwa baada ya umoja huo, unaoundwa na nchi zaidi ya 40 kukubaliana kwa pamoja makao makuu yake yajengwe Tanzania, mkoani Arusha.

"Baada ya makubaliano hayo Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Julius Nyerere alitoa eneo hili mwaka 1980, lakini miaka imepita kwa sababu mbalimbali, lakini Rais John Magufuli amehakikisha maono hayo yanatimia na sasa ujenzi unaanza tunamshukuru sana," alisema.

Aliahidi kuja mara kwa mara inavyowezekana kuangalia maendeleo ya ujenzi huo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), James Kilaba, alisema kuanza kwa ujenzi huo ni furaha na fursa kwa Watanzania.

Alitoa wito ujenzi huo ufanywe kwa weledi na kwa kuzingatia mkataba uliopo.

Msimamizi wa mradi huo kutoka kampuni ya B.J.Amuli Architects, Nathanael Alute, aliahidi kusimamia ujenzi huo ili ukamilike kwa wakati.

Katibu Mkuu Msaidizi wa PAPU, Kolawole Raheem Adulo-ju, alimshukuru Rais John Magufuli kuweka historia kwa kuhakikisha ujenzi huo unafanyika baada ya miaka mingi kupita.

Wakati ujenzi huo ukianza rasmi Januari 8, mwaka 2020, PAPU inatarajia kuadhimisha miaka 40 tangu kuanza kwa umoja huo mkoani Arusha Januari 17 na 18 mwaka huu.

# Waziri aagiza viongozi TCCCo wakamatwe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, ameagiza kuchukuliwa hatua kwa viongozi wa kiwanda cha kukoboa Kahawa cha Tanganyika (TCCCo) kilichopo Moshi, kwa tuhuma za kushindwa kulipa fedha zaidi ya Sh. milioni 150.

Fedha hizo ni za wakulima wa kikundi cha Kalinzi Organic Coffee kilichopo mkoani Kigoma, za msimu wa zao hilo wa mwaka 2011/2012. Waziri huyo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kukutana na uongozi wa kiwanda hicho, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, la Julai 30, 2018, alipotembelea shamba la kahawa katika Kata ya Nyarubanda, wilayani Kigoma.

Waziri Mkuu alimtaka Naibu Waziri kufuatilia Sh. milioni 150 walizotakiwa kulipwa wakulima wa kahawa wa Chama cha Msingi cha Kalinzi Organic Coffee Grower zilizolipwa kwenye kikundi kingine licha ya wakulima hao kuuza kahawa yao. Alisema alilazimika kuchukuwa hatua hizo baada ya uchunguzi na kubaini kuwa fedha hizo zililipwa kimakosa na Bodi ya Kahawa (TCB) kwenda kwa Chama cha Msingi cha Kalinzi Farm Coffee badala ya Chama cha Kalinzi Organic Coffee Grower ambao ndio waopeleka kahawa kwenye kiwanda hicho. "Tumechunguza tumejiridhisha fedha hizo zililipwa kimakosa kwa Chama cha Msingi cha Malinzi Farm Coffee badala ya Chama cha Kalinzi Organic Coffee Grower, lakini viongozi waliokuwapo madarakani hawakuchukua hatua zozote kwa kipindi cha miaka minane sasa," alisema.

Aidha, alisema katika msimu wa mwaka 2011/2012, kikundi cha wakulima wa kahawa cha Kalinzi Organic Coffee kilichopo mkoani Kigoma kiliwasilisha kahawa yao kukobolewa TCCCo, lakini fedha zilipelekwa katika kikundi kingine jambo ambalo serikali ya awamu ya tano haitalifumbia macho.

Meneja wa TCCCo, Japhet Ndosi, amekiri kukobolewa kwa kahawa ya Kalinzi Organic Coffee, lakini uongozi wa wakati huo ulijaza jina tofauti la kikundi kwenye fomu inayopelekwa kwenye mnada kwenye bodi hiyo.

"Ni kweli makosa hayo yalifanyika hapa kwetu na viongozi waliokuwapo madarakani kipindi hicho hivyo viongozi hao kwa kushirikiana na waliopokea fedha wawajibishwe ili wakulima waweze kupata haki yao," alisema Ndosi.



Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba (kushoto), akikagua moja ya bustani ya miche ya kahawa katika taasisi ya tafiti ya Kahawa (TaCRI), mkoani Kilimanjaro jana. Kulia ni mtafiti wa taasisi hiyo, Sofia Malinga. **PICHA: MARY MOSHA**

# Vunjo walilia ukarabati barabara

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wakazi wa vijiji vinne katika Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Wilaya ya Moshi, wameomba serikali kukarabati barabara ya Kongo hadi Manu kutokana na kutopitika nyakati za mvua.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Janispher Nyambo alisema kipindi hiki cha mvua wanapata adha kubwa huku baadhi ya wajawazito wakishindwa kwenda hospitali kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Naye Clementina Dominic, alisema nyakati za mvua kinamama wajawazito na watoto wadogo hukumbwa na adha kubwa kwa kutumia usafiri wa bodaboda kutokana na baadhi ya magari kutoweza kufika hali ambayo inahatarisha maisha yao. Alisema ni vyema hatua zikachukuliwa haraka ili kuwawezesha wananchi kupata huduma muhimu za kijamii ikiwamo kusafirisha mazao yao.

"Tunaelekea katika kipindi cha masika, tunaomba serikali kuangalia kwa jicho la pekee barabara hizi zinahatarisha maisha ya kinamama hasa nyakati za usiku wanapopata uchungu na watoto wanapougua usiku," alisema Jamila Mussa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Manu, Joseph Chaki, alithibitisha kuwapo kwa changamoto nyakati za mvua za vuli na masika katika barabara hiyo, na kwamba wameanza kuchangisha wananchi ikiwa ni pamoja na wazaliwa wa vijiji hivyo waishio nje ya Mkoa wa Kilimanjaro.

"Barabara ya Kongo hadi Manu yenye takribani kilomita sita inayounganisha vijiji vya Mare, Kanango, Manu na Yamu imekuwa hadha kwa wakazi wa vijiji hivyo hali inayokwamisha maendeleo ya wananchi," alisema.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Roy Johansen, alisema barabara hiyo imeingia kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 na kwamba itatengenezwa kwa kilomita nne za changarawe.

"Tunawaomba wananchi kuwa wavumilivu na ikiwa kuna kikundi cha watu wanaotaka kuanza ujenzi kabla ya mvua kuanza, afike osifini kwetu na tutawapa ushirikiano wa hali ya juu," alisema.

## Wakulima mpunga Moshi walilia soko

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WAKULIMA wa mpunga wa skimu ya Kivulini Wilaya ya Mwanga, wamelalamikia kukosa masoko ya uhakika ya mazao yao hali iliyosababisha kupata hasara kubwa kutokana na walanguzi kununua kwa bei waitakayo wao.

Wakulima hao wa skimu hiyo yenye ukubwa hekari 900, wamejikuta kwenye tafakari namna ya kuendelea na kilimo kwa msimu ujao kutokana na mpunga huo kununuliwa kwa lumbesa pamoja na kupanda bei kwa pembejeo za kilimo huku wakisubiriwa na mahitaji ya familia.

Wakizungunza na Nipashe jana, Nangera Juma, alisema baadhi wanapeleka mpunga mashine ili kuongezea thamani na kuuza kama mchele huku wengi wao wanashindwa kumudu gharama za ukoboaji na kulazimika kuuzia mashambani ambapo wafanyabiashara wananunua kwa gharama ndogo na baadaye kukoboa na kuuza mchele kwa faida kubwa.

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wakulima ili wapate masoko ya uhakika yatakayowasaidia kujikwamua na umaskini na kuingia kwenye uchumi wa kati kwa Mtanzania mmoja mmoja," alisema Azizi Mchomvu na kuongeza:

"Serikali ya mkoa iangalie namna ya kuwatoa wataalamu wa wakala wa vipimo ofisini na kwenda kwa wakulima ambao kwa sasa uuzaji wa mazao kwa mfumo wa lumbesa umeanza tena, huku wao wakiutazama na kufanya kazi zao wakiwa maeneo ya ofisini tuu."

Mtaalamu wa zao la mpunga wa Chuo cha Kilimo KATC Moshi, Emanueli Makuninda, alisema wameanza mradi wa usimamizi na udhibiti ubora wa zao la mpunga ili wakulima wa skimu hiyo walime mpunga utakaokuwa na ushindani kwa masoko ya ndani na nje ya nchi na kupata masoko ya uhakika ili kuepuka kulanguliwa.

"Tumeanza mradi wa usimamizi na udhibiti wa ubora wa mpunga kuwajengea uwezo wakulima kulima kwa kiwango kitakachokubalika kwenye soko la ndani na nje ya nchi ikiwa hii ni mbinu pekee ya kuepukana na ulanguzi wa soko na kujikimu kimaisha wakati serikali inaendelea kushughulikia upatikanaji wa soko la uhakika," alisema Makuninde.

Aidha, msimamizi mkuu wa mashine ya kuongeza thamani ya zao la mpunga, Juma Daudi, alisema kwa siku mashine hiyo ina uwezo wa kukoboa magunia 30 hadi 50, lakini wakulima wengi hawana uwezo wa kutumia mashine hizo.

"Wakulima wanalalamika kukosekana kwa soko hili ni kutokana na wengi wao hukoboa mpunga wao kwa kutumia mikono, hali ambayo inachangia takataka nyingi na kupoteza upora wa mchele katika soko," alisema Juma.

# ama

ALHAMISI JANUARI 9, 2020

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**Ugonjwa akili, fumbo linaloipa jamii mtihani**



Ukurasa 18

Ujenzi bora vituo vya tiba Mbeya vyamtembeza Jafo kwa tabasamu




Ukurasa 17

**Vifusi vya satelaiti ya India vyataabisha 'wenye dunia'**



# Bajeti Lishe Kagera bado shida

Ukurasa 16



Mgonjwa akitibiwa mjini Wuhan. **PICHA: MTANDAO.**

# Homa ya ajabu yazuka nchini China

**WUHAN,** China

MAMLAKA zinazohusika na afya nchini hapa, zimeanza kuumiza vichwa kutokana na kuibuka ugonjwa wa ajabu, unaofananishwa na homa ya mapafu.

Hadi kufikia mwisho wa wiki, katika jiji la Wuhan tayari kulikuwapo wagonjwa 44, kati yao 11 walikuwa katika hali mbaya zaidi.

Ni hali iliyozua hofu katika nchi jirani za Singapore na Hong Kong, ambazo imeanzishwa ukaguzi mkali kwa wageni wanaoingia katika nchi yao, hofu ni kujihami wasipate maambukizi hayo.

Inakuwa mkasa mwingine, kwani kati ya mwaka 2002 hadi 2003, yaliibuka maambukizi ya maradhi yanayofanana na hali ya sasa na uliua jumla ya watu 700 duniani kote, chanzo chake ni nchini China.

Mamlaka za afya mjini hapa, zinafanya uchunguzi kujua undani wa mkasa ulivyo na kasha unakagua maradhi mbalimbali, yakiwamo mafua.

Jambo moja lililofahamika kwa mujibu wa mamlaka hao wa kiafya, ni kwamba sehemu kubwa ya wagonjwa wa sasa wanatumikia katika maeneo kunakouzwa bidhaa za vyakula vya majini kama vile samaki.

Msemaji wa Shirika la Afya Duniani, (WHO), alisema tayari shirika linafuatilia kinachoendelea na lipo katika mawasiliano ya karibu na serikali ya China, kujua kinachoendelea.

AFYA

# Ugonjwa akili, fumbo linaloipa jamii mtihani

• Pata mkasa wa kilichojiri kwa familia




Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, Batabika nchini Uganda.



Esther Kiama, anayepata madhila kutokana na maradhi ya mumewe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Mwandishi Wetu**

MAGONJWA ya akili yameongezeka kwa kasi katika jamii, ikiwamo ukanda wa nchi za Afrika Mashariki. Ukipita mitaani utawaona watu walioathirika na matatizo hayo walivyozagaa, bila kupata usaidizi wowote.

Wengi wanafananisha magonjwa ya akili sawa na tabia ya utumiaji wa dawa za kulevya, imani za kishirikina na wengine wanadai ni tamaa za kupata mali.

Kisa kimoja kilichotokea nchini Kenya, ni uthibitisho kwamba jamii inapaswa kuangalia upya mitazamo yao kuhusu ugonjwa wa akili ili kulinda umoja na mshikamano ndani ya familia.

> Sisi hatupendi kusema kuwa mtu ni wazimu, ila kama wanasaikolojia hutizama ishara anazoonyesha mgonjwa, na kutathmini ni ugonjwa upi wa kiakili anaougua mgonjwa.

### MKASA WA KENYA

Esther Wanjiru Kiama, ambaye alidumu katika ndoa na mume wake kwa muda wa miaka 10, alijikuta akiishi kama mfungwa kutoka familia ya mume kumtenga.

Esther (60) na mumewe, David Kiama Kuru, wana watoto wanne na wajukuu sita.

Pamoja na kuishi kwa muda mrefu, ndoa yake ilikabiliwa na majaribio, wakati mumewe alipoamua kwenda kutafuta riziki mbali na familia yake.

Kuru alikwenda magharibi mwa Kenya ambako alifanya kazi huko kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Ni baada ya kipindi hicho ndipo, alipopokea simu ya ghafla akitakiwa kufika mjini Bungoma mara mmoja na huko alipewa ufafanuzi kwamba mumewe amepatwa na ugonjwa wa akili.

Kuanzia hapo, Esther anasema maisha ya jamii yake yalianza kubadilika, sababu mume wake alikuwa ndiye tegemeo la riziki ya familia, hivyo walianguka kiuchumi.

Anasema alishtuka sana kumuona mumewe akiwa amechanganyikiwa, haelewi mambo yaliyokuwa yanaendelea. Alikuwa katika ulimwengu wake mwingine.

Esther an ahoji kuwa awali ilikuwa vigumu kuelewa ni ugonjwa upi aliokuwa anaugua mumewe, kwani alikuwa na ishara za kuchanganyikiwa akijisemesha mwenyewe.

Kuanzia hapo, Esther anasema baadhi ya marafiki zake, jamaa na walianza kumsema na kumsimanga kwamba, yeye Esther ndiye chanzo cha maradhi anayougua mumewe wake.

"Waliniita majina mengi... kuwa mimi ndio nimemroga mume wangu, " anasimulia Esther.

### TIBA YA MUME

Licha ya mapitio hayo, aliamua kujipa nguvu na kufunika aibu ya mumewe, hivyo haikuwa rahisi kwani jamaa wa kutoka upande wa mumewe. Kuna siku walimchukua kwa nguvu ndugu yao na kumsafirisha hadi kwao vijijini, wakiwa na imani Esther hakuwa na nia mbaya kwa mume.

Kwa miaka mitatu yeye na wanawe walitafuta njia ya kumuona Kuru, lakini familia ya mumewe ilimpiga marufuku.

Kilikuwa kipindi kizito mno kwa Esther, japo hakukata tamaa. Baada ya miaka mitatu, Esther alitafuta njia ya kumtoa kwa nguvu mumewe kutoka mikononi mwa jamii yake, alipanga njama na watoto wake ambayo ilifaulu.

"Nilipomuona mume wangu sikuamini macho yangu... afya yake ilikuwa imedhoofika sana kana kwamba hakuwa na mtu wa kumuhudumia ipasavyo," anasema Esther.

Anasema kuwa kucha za miguu na za mikono zilikuwa ndefu na ngumu, ilichukia siku kadhaa kuzisafisha.

"Ni vigumu sana kumtizama mtu unayempenda akihangaika na ugonjwa usiouelewa vyema, ila nilijizatiti tu," anaongezea Esther.

Baada ya kumrejesha nyumbani, safari ilianza ya kumtunza na kuhakikisha kuwa mume wake anapata matibabu ya hospitalini.

### USHIRIKINA?

Mwanasaikolojia anayehusika na saikolojia, Daktari Maggie Gitu, anasema kuwa sio sawa kwa jamii kuwaona wagonjwa wenye matatizo ya akili kama wamerogwa au wanatumia dawa za kulevya.

Daktari Gitu anasema kuwa magonjwa mengi ya kiakili hutokea pale kemikali kwenye ubongo wa mgonjwa inaposhuka sana na ubongo kushindwa kuhimili kazi yake ya kawaida.

Magonjwa mengi ya kiakili husababishwa na hali ya mtu za kiindani, husukumwa na hisia za upweke, hofu au kuhisi kana kwamba hupendwi au hakuna anayekuthamini.

Anafafanua kwamba ugonjwa wa akili hutokea pale mtu anapohisi kana kwamba amefeli kulifikia jambo fulani katika maisha yake na kuishia kupoteza uwezo wake wa kufikiria.

Njia inayotumiwa sana mbali na kutoa ushauri wa ndani kwa wagonjwa wa kiakili, ni matibabu ya kutumia dawa tofauti ambazo wagonjwa humeza katika kipindi fulani kama njia ya kuihimili hali.

Tangu mwaka wa 2017, mumewe Esther Kiama alianza kuonyesha dalili za kupona kufuatia matibabu aliyokuwa anapokea licha ya kuwa bado anatumia dawa hizo hadi sasa.

***• Kwa msaada wa mtandao***

AFYA

# Huu ndio mtindio wa ubongo, chanzo na dalili zake zilivyo

Na Mwandishi wetu

UNAUJUA mtindio wa ubongo? Hili ni tatizo linalotokana na mfumo wa fahamu na kitaalamu inaitwa 'uneurologia' ikihusisha na kiungo hicho na mishipa ya fahamu.

Tatizo hilo linalojitokea mara mtoto anapozaliwa, huathiri sehemu ya ubongo unaohusika na misuli ya mwili.

Ni tatizo linalotokea, pale ubongo haujakamilika katika ukuaji wake au kupata shida wakati wa kujifungua.

## KWANINI HIVYO?

Kuna sababu nyingi za mtindio wa ubongo, lakini wataalamu wa magonjwa ya akili wanakubali kwamba vyanzo vifuatavyo husababisha matatizo hayo kwa wingi.

Maambukizi anayopata mama wakati wa ujauzito, huleta hatari kwa mtoto kupata mtindio wa ubongo pale anapozaliwa.

Mama kupata matatizo wakati wa kujifungua kama kumbana mtoto au kutumia muda mrefu wakati wa kujifungua na kujifungua kabla ya wakati huchangia tatizo hilo.

Kutokwa kwa damu kwenye ubongo wa mtoto na kubadilika kwa mfumo wa vinasaba pia zinaweza kuathiri ukuaji wa ubongo wa mtoto.

## DALILI ZAKE

Dalili za mtindio wa ubongo, kwa kawaida huonekana sana katika kipindi cha umri wa miaka mitatu ya mwanzo ya ukuaji baada ya kuzaliwa.

Dalili hizo ambazo wazazi wanatakiwa kuwa makini kufahamu ni kama kukaza kwa misuli au misuli ya mwili kushindwa kufanya kazi na kulegea au kuishiwa nguvu kwa misuli. Pia mtoto ataonekana kutokuwa na uwezo wa kuzuia na kuufanya mwili anavyotaka.

Tahadhari ni kwa wazazi wanapaswa kuwa makini kwani dalili hizi zinazoweza kuonekana sehemu mbalimbali za mwili na inategemea kiasi gani mtoto kaathiriwa, na tatizo hilo.

Wengine wanaweza kuwa na matatizo madogo na baadhi inawafukisha mbali, hadi kupata ulemavu wa baadhi ya viungo vya mwili. Watu wengi wenye mtindio wa ubongo huwa wanapata matatizo mengine kama kifafa wakati mwingine, pia wanashindwa kutafuna, hata kumeza chakula.

Tatizo linapokuwa kubwa mwathirika hawezi kuongea na kupata choo kigumu au kwa shida.

Athari nyingine inayoweza kuonekana, ni kutoweza kuzuia mkojo kutoka, matatizo ya kuona na kusikia, matatizo ya kiunzi kama kupinda kwa uti wa mgongo na mifupa kukaa sehemu tofauti kama mfupa wa paja.



Ndivyo ilivyo huduma na msaada kwa wenye mtindo wa ubongo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Watoto hawa wanahitaji kuonyeshwa upendo na kusikilizwa, ingawa inaweza kuwepo changamoto ya kutambua watoto wenye tatizo hilo wakiwa wadogo.**



## UTAGUNDUAJE?

Pindi tu unapogundua kuwa maendeleo ya mtoto wako sio mazuri katika ukuaji wake, basi muone daktari haraka ili kujua ni nini tatizo.

Daktari anaweza akamfanyia uchunguzi kitaalamu na kujua tatizo liko wapi. Pia, anaweza akatumia vipimo mbalimbali vya kitabibu hospitalini, kubaini tatizo kama Ultrasound Scan, Magnetic Resonance Imaging ( MRI), Computerized Tomography(CT) Scan, Electroencephalogram ( EEG) na Electro myogram( EMG).

Watoto wote wenye matatizo haya ya mtindio wa ubongo wanaweza pia kujifunza kusoma au kufanya mambo mbalimbali iwapo watapewa msaada maalum na kuandaliwa mazingira mazuri yatakayowashawishi kujifunza.

Malezi kwa watoto wenye matatizo hayo, yanatakiwa yawe tofauti na yale ya watoto wa kawaida.

Watoto hawa wanahitaji kuonyeshwa upendo na kusikilizwa, ingawa inaweza kuwepo changamoto ya kutambua watoto wenye tatizo hilo wakiwa wadogo.

Huwa vigumu mzazi au jamii kumtambua mtoto mwenye tatizo la mtindio wa ubongo hasa akiwa na umri chini ya miaka minne.

Mtoto mwenye mtindio wa ubongo anafundishika, iwapo tu atafundishwa kwa makini, utulivu na uvumilivu mkubwa.

Kama ni mwalimu, anatakiwa awe mpole na ufundishaji wake na asiwe wa haraka, bali aonyeshe mapenzi kwa mwanafunzi huyo mtoto. Watoto wa aina hiyo, wanashauriwa wapewe nafasi ya kujenga urafiki na watoto wenzao wa rika lao ili weweze kujifunza baadhi ya mambo yanayowezekana kulingana na uwezo wao wa kujifunza.

Iwapo mtoto mwenye ugonjwa huu atatengwa na wenzake, hali hiyo itamsababishia kutokuwa na maendeleo ya kuweza kufanya jambo lolote. Wataalamu wanakushauri watoto hao wachanganywe na wenzao, na kuachana na tabia ya kuwatenga na au kuwafungia ndani.

Mara nyingi mtoto mwenye tatizo hili anaweza kupata msaada wa mazoezi ya viungo na mazoezi mengine mepesi yatakayomsaidia kuendelea na maisha kama walivyo watoto wengine.

## USHAURI

Wazazi wanashauriwa pale wanapozaa mtoto mwenye tatizo hili kumchukulia kuwa ni mtoto kama walivyo watoto wengine ili kuiwezesha jamii inayomzunguka kumchukulia kawaida.

Wazazi wanatakiwa kuonyesha ushirikiano na kuonyesha upendo kwa mtoto huyo na sio kumtenga kama ilivyo kwa wazazi wengine wanaofikia hatua ya kufarakana kwa kuona kama mikosi au laana.

***Ni kwa msaada wa mtandao***

AFY A

# Bajeti Lishe Kagera bado shida

## • Halmashauri 'zachenga' agizo • Bukoba, Kyerwa, Karagwe pekee waliofanikiwa • Simulizi tabu ya Missenyi ilivyo



Wazazi na walezi kutoka Kata ya Buyango, wakiwa katika Tamasha la Mtoto Mwerevu, Zahanati ya Buyango, Missenyi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

HALMASHAURI tano kati ya nane za mkoa wa Kagera zimeshindwa kutekeleza bajeti ya Sh. 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano, katika bajeti iliyopita, ikilenga kukabiliana na tatizo la lishe duni kwao.

Utaratibu wa halmashauri kutenga fedha hizo kutoka mapato ya ndani ya halmashauri, ulianzishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa lengo la kupambana na hali duni za watoto.

Miongoni mwa halmashauri zilizoshindwa kutekeleza bajeti hiyo mkoani hapa ni Missenyi ambayo kati ya Sh. milioni 38 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, mpaka mwaka unakwisha, zilizotolewa kwa ajili ya kuhudumia watoto wenye lishe duni ni Sh. milioni 5.3.

**OFISA LISHE (M)**

Ofisa Lishe Mkoa wa Kagera, Yusuph Hamis, anasema kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 halmashauri tatu pekee zilizovuka asilimia 50 ya fedha zilizolengwa kutengwa katika bajeti.

Anataja viwango vyao katika mabano ni Bukoba (61.8%), Kyerwa (60%) na Karagwe (57%) na zile ambazo hazikufanya vizuri ni Manispaa ya Bukoba iliyotenga asilimia 21, Missenyi (15%), Muleba (3%), huku Biharamulo na Ngara hazikutenga kabisa bajeti hiyo.

"Halmashauri ya Wilaya ya Ngara haikutoa kabisa fedha hizo, lakini sababu wanayoitaja ni kuwa 'afueni' zilizopangwa zilionekana zimepangwa, pia kutekelezwa na wadau na hii ni kutokana na kutofuatilia wakati wa upangaji," anasema.

Hamisi anataja sababu kubwa za halmashauri kushindwa kutoa fedha kama zilivyotengwa, ni masuala ya lishe kutopewa kipaumbele.

Kuhusu hatua zinazochukuliwa, anasema kuna jitihada mbalimbali zinafanyika, ikiwamo vikao na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliyeagiza kuwa fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati, kutekeleza malengo.

"Tumefanya vikao na halmashauri na sasa msukumo ni mkubwa na wakurugenzi wameahidi watatoa kipaumbele," anasema.

**HALI MISSENYI**

Hadi sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, inakabiliwa na tatizo la watoto wenye lishe duni, huku upimaji ukiendelea na vijiji viwili zimeshathibitisha.

Katika vijiji vya Buchurago na Bugorora, imebainika kati ya watoto 535 wenye umri wa chini ya miaka mitano waliopimwa, watoto 51 walibainika kuwa na utapiamlo wa kadri, huku watoto 35 wana utapiamlo mkali.

Hata hivyo, pamoja na changamoto hiyo shughuli za kukabiliana na lishe duni zimeendelea kufanyika kwa kutumia sehemu ndogo ya bajeti iliyotolewa na fedha za wafadhili, kuhakikisha afya za watoto wenye lishe duni zinaimarika.

Takriban mwaka mmoja uliopita, watoto 30 katika kijiji cha Bugorora walipimwa na kukutwa wakiwa katika kinachoitwa 'rangi nyekundu' katika kadi zao kliniki, hali iliyosababisha kuwekwa kambi ya kunusuru afya za watoto hao.

> **Takriban mwaka mmoja uliopita, watoto 30 katika kijiji cha Bugorora walipimwa na kukutwa wakiwa katika kinachoitwa 'rangi nyekundu' katika kadi zao kliniki, hali iliyosababisha kuwekwa kambi.**



Mama Geniva Ereneus (30), mwenye watoto mapacha Oliva na Olivia Ereneus, akiendelea kuwalisha chakula dawa katika Tamasha la Mtoto Mwerevu Kata Buyango, wilayani Missenyi.

**NENO WAZAZI**

Sumaida Mustapher, ni mkazi wa kijijini Bugorora na mama wa watoto wanne, ni miongoni mwa wazazi ambao watoto wao walipimwa na kubainika hali duni kiafya.

Mama huyo anasema ya kuwa wakati anaambiwa mtoto wake ana lishe duni, alikuwa na umri wa miaka minne na uzito wa kilogramu kumi na moja, na kuwa aliambiwa kwa umri wa mtoto wake ingebidi awe na kilogramu kati ya 14 hadi 15.

Anasema baada ya kubaini hali hiyo aliwekwa katika kambi ya kufundishwa namna ya kuandaa na kumlisha mtoto kwa zaidi ya miezi mitano na sasa mtoto ana miaka minne na miezi mitano na ana kilo 16.

"Miongoni mwa vyakula nilivyofundishwa kuandaa ni dagaa, karanga na unga wa dona, ambao nampikia mtoto uji na kumnywesha kutwa mara tatu, pia nilifundishwa kumpa mboga za majani na matunda ninayoweza kuyapata kulingana na kipato changu," anasema.

Hata hivyo, mama huyo anakiri hakuwa na taratibu wa kumuanzisha mtoto wake kumpa vyakula vingine, kabla ya kutimiza miezi sita, badala ya maziwa ya mama pekee, inavyotakiwa kiafya.

Mzazi Yudes Wilbard, kutoka kijiji hicho ana watoto watatu na kati yao, wa pili alipimwa na kubainika na uzito pungufu kutokana na kuwa na lishe duni.

Anasema mtoto alikuwa na umri wa miaka miwili na miezi sita, wakati huo akiwa na uzito wa kilo tisa na kuwa kwa sasa ana miaka mitatu na uzito wa kilo 12.5.

"Mtoto wangu anaendelea vizuri, nikilinganisha na kabla ya kupata elimu ya namna ya kumwandalia chakula," anasema.

**MHUDUMU AFYA**

Mhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Kijiji cha Bugorora, Odiro Adrian, aliyepata mafunzo ya namna ya kuwapima watoto na kubaini wenye lishe duni, namna ya kuwaandalia chakula na kuwalisha ana maoni yake anachojifuza kazini.

Odiro anasema, huwa anafanya kazi hiyo kwa kutembea 'nyumba kwa nyumba' na kwamba baada ya kuwapima na kuwabaini, anawafundisha kuwalisha na kuwanyonyesha watoto hao.

"Pia, tunawaelimisha wajawazito na wote tunawaorodhesha na kuwatembelea mara kwa mara, ili kuangalia maendeleo yao," anasema.

> **Mtoto wangu anaendelea vizuri, nikilinganisha na kabla ya kupata elimu ya namna ya kumwandalia chakula.**

Odrian anasema, ni takariban mwaka mmoja sasa, tangu awapime watoto katika kijiji hicho na kubaini kuwapo watoto 30 wenye lishe duni na hatua za kuwasaidia zinaendelea kliniki.

Baada ya kuwabaini, waliandaa kambi maalumu ya kufundisha wazazi wa watoto hao namna ya kuandaa chakula cha watoto wao na kila baada ya miezi mitatu wanawapima ili kuona maendeleo ya watoto hao.

"Sasa watoto wengi wanaendelea vizuri katika kadi zao za kliniki wamekwishaingia katika rangi ya

INAENDELEA UK.20

# Vifusi vya satelaiti ya India vyataabisha 'wenye dunia'

KISIASA, kuna mgongano kati ya Pakistani, inayoshutumu mpango wa safari za majirani India, kuwa chanzo cha vifusi katika anga za mbali duniani.

Hayo yanatokea, huku Waziri wa Sayansi na Teknolojia wa India, Fawad Chaudhry, akikiri nchi yake kuhusika na uchafuzi wa anga za juu.

Vifusi vya anga za juu, ni mamia ya vipande vilivyomeguka kutoka sehemu za roketi kuu au kwenye satelaiti, vinavyochafua anga za juu, hususan katika uzio wa dunia (obiti).

Kauli ya Chaudhry, ni sehemu ya kujibu ripoti ya uvumbuzi uliofanywa na Shirika la Anga za Juu la Marekani, Nasa, kuwapo vifusi kutoka chombo cha anga za mbali cha India kilichoanguka kwenye Mwezi Septemba mwaka huu.




Kifaa cha satelaiti mali ya India. **PICHA: MTANDAO**

**UCHAFUZI ANGANI**

Inaelezwa kuwapo vipande zaidi ya 23,000 vya vifusi ambavyo ni vikubwa kuliko sentimita 10 (inchi nne) na Shirika la Nasa, liliona vifusi vingi vilivyoko katika umbali wa maili 1,250 kutoka iliko uso wa dunia, kazi inayofanywa na satelaiti gushi zaidi ya 2,000.

Kitaalamu inatafsiriwa, kuna uwezekano mkubwa wa mgongano kutokea, sehemu kubwa ikiwa kati ya vifusi vilivyopo sasa vitokanavyo na migongano ya sasa katika anga za juu.

China ilipofanya jaribio katika moja ya setilaiti zake za hali ya hewa mwaka 2007, inaelezwa ilitengeneza vifusi vilivyokadiriwa kuwa 3,000.

Aidha, mgongano utokanao na ajali ya satelaiti za mawasiliano za Marekani na Russia mwaka 2009, nazo ziliongeza idadi ya vipande vikubwa vya vifusi katika obiti.

**KIWANGO CHA INDIA**

Kwa kuoanisha takwimu za utengenezaji uchafu wa anga za juu, India bado inazalisha kiwango cha chini, kuliko nchi tatu zenye kiwango cha juu cha uchafuzi wa mazingira ya anga za juu, ambazo ni Russia, Marekani na China.

Vifusi vilivyotengenezwa na India, vimeongezeka kutoka vipande 163 mwaka 2019 hadi 117 mwaka 2018.

Mwezi Machi mwaka huu, India ilikuwa nchi ya nne kufanya jaribio la kombora la kulipua satelaiti na inaitetea kuhusu usalama kwamba, kama kungekuwapo na madhara, pindi tu kipande chake katika majaribio hayo, chombo hicho kingesalia duniani.

Hata hivyo, Marekani inalaani urushaji huo, huku Taasisi ya Nasa kupitia mitambo yake inasema iliona vipande vipatavyo 50 vilivyomeguka kutokana na jaribio hilo, ikiwa ni zaidi ya mara tatu baada ya ilipofanyika.

"Ikiwa vitendo vya China vya zaidi ya muongo uliopita vilikuwa ni vibaya zaidi, India ambayo ilitengeneza vifusi zaidi hivi karibuni ingepaswa kujua kuwa inafanya kitu kinachomwathiri kila mmoja," anasema Christopher Johnson.

Mwanasheria huyo ambaye ni Mshauri wa Sheria wa Anga za Mbali katika Wakfu wa Uhifadhi wa Mazingira ya Anga, wenye makao yake nchini Marekani, anaendelea:

"Tunastahili kujifunza kutokana na matukio yaliyopita na kutambua kwamba hakuna haja yoyote ya kusababisha vifusi katika anga za juu, ambavyo vinatishia kila mmoja kutumia anga ya mbali."

Malalamiko yaliyoko ni kwamba, hadi sawa duniani kunashuhudiwa maandalizi ya maelfu ya setilaiti, huku nyingine nyingi zikiendelea kupangwa kurushwa, hali inayoongeza uwezekano wa kugongana na hakuna sheria ya kimataifa inayodhibiti majaribio hayo.

Nchi kadhaa na kampuni ya kibinafsi zinafanya majaribio ya mbinu mpya, kupunguza athari za vifusi vya kwenye anga za juu, ikiwamo sumaku hadi nyavu.

Mwaka 2025, inatarajiwa Nasa itazindua satelaiti yake ya kwanza kuondoa vifusi kutoka kwenye mzunguko wa dunia na inasema, uondoaji vifusi hivyo kwenye anga bado changamoto inayootafsiri kuwa ya kiuchumi na kiufundi.

**Kwa mujibu wa taarifa za mtandao.**

AFYA

# Ujenzi bora vituo vya tiba M vyamtembeza Jafo kwa taba

• Ufisadi Chunya wamkatiza kicheko • Aungana na RC huruma



Kituo cha Afya cha Masukulu, wilayani Rungwe. **PICHA: MAKTABA**

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBEYA ni miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri kwenye utekelezaji wa Sera ya Afya ya Mwaka 2008, inayotaka kujengwa kwa zahanati katika kila kijiji, kituo cha afya cha kata na wilaya kuwa na hospitali, huku hospitali ya mkoa kuwa ya rufani.

Kwa sasa mkoa huo una wilaya sita na halmashauri saba, ambazo kila moja ina hospitali yenye hadhi ya wilaya zaidi ya moja, isipokuwa halmashauri za Chunya na Busokelo, ambazo kila moja ina hospitali moja.

Taarifa ya Sekta ya Afya iliyowasilishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Novemba 27 mwaka jana, inasema hadi kufikia mwezi Oktoba mwaka jana, mkoa ulikuwa na vituo vya kutoa huduma za afya 323.

Mchanganuo wake ni zahanati zilikuwa 282; vituo vya afya 25 na hospitali 16, zinazomilikiwa na serikali, watu binafsi na taasisi za dini. Tangu serikali ilipoanza kutekeleza miradi ya afya kwa kutumia mfumo wa Account ya dharura (Force Account), unaiohamasisha matumizi ya mafundi wa mitaani badala ya makandarasi, katika mkoa wa Mbeya vimejengwa vituo vya afya 14.

Baadhi ya vituo hivyo vimeshakamilika na vinaendelea kutoa huduma na baadhi vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi, serikali ikishirikiana na wananchi katika kila hatua ya ujenzi.

Hadi sasa serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya katika halmashauri tatu, ambazo ni Mbarali, Busokelo na Wilaya ya Mbeya, ambazo kila moja ilipatiwa fedha Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

> “Wilaya hii ina kanda kuu mbili, ambazo ni ukanda wa kilimo na ukanda wa madini. Sasa ina ongezeko kubwa la watu kiasi kwamba hospitali hii ya wilaya haikidhi mahitaji.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo (katikati), akizungumza na wananchi wa Kata ya Chalangwa, wilayani Chunya katika Kituo cha Afya cha Kata hiyo, alipokuwa ziarani. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

### ZIARA YA JAFO

Hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alifanya ziara katika maeneo mbalimbali ya Mkoa Mbeya, lengo nia kukagua maendeleo ya miradi mbalimbali iliyo chini ya wizara yake.

Katika ziara hiyo alitembelea zaidi miradi ya afya na kwa kiwango na elimu, pamoja na kufanya mazungumzo na watumishi wa halmashauri alizotembelea.

### MBARALI

Ni ziara iliyoanzia wilayani Mbarali, ambako alikagua mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya, ambayo awali ilikuwa inasuasua kutokana na sababu mbalimbali, mpaka Rais John Magufuli, alipoagiza ujenzi huo kukamilika haraka.

Waziri Jafo alikiri kufurahishwa na kasi ya ujenzi wa majengo ya hospitali hiyo na viwango vyake na alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwa kushirikiana na watendaji wa halmashauri hiyo, kuendelea kusimamia viwango, ili thamani halisi ya fedha zilizotolewa ionekane.

Jafo alionyesha furaha zaidi, alipopewa taarifa na Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune, kuwa hospitali imekamilika kwa asilimia 98

# lbeya asamu

## a hospitali yao








Majengo ya Kituo cha Afya Ikuti, wilayani Rungwe, ambacho ndicho kioo cha ubia wa kazi za wananchi. **PICHA: MAKTABA**

na sehemu chache ikiwamo urekebishaji baadhi ya milango na aliahidiwa haitachukua muda mrefu kukamilishwa.

Vilevile Waziri Jafo, alisema taarifa alizo nazo kuhusu ujenzi wa hospitali zingine za wilaya katika mkoa huo ambazo ni Hospitali ya Wilaya ya Mbeya na Busokelo ni nzuri na ujenzi unazingatia maelekezo ya wizara, hivyo aliahidi kuongeza fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

"Nimefurahishwa sana kwa jinsi mnavyosimamia ujenzi wa hospitali hizi. Sasa zipo Sh. bilioni 1.5 ambazo zitaongezwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hizi, ili zianze kufanya kazi haraka, kila moja italetewa milioni 500 na nina imani zitatosha," anasema Waziri Jafo.

Aidha, baada ya kutoka katika Hospitali ya Mbarali, alitembelea Hospitali ya Wilaya ya Mbeya, inayojengwa katika Kata ya Inyala, ambako ujenzi wake ulianza mapema mwaka 2019 na mpaka sasa ynaelekea kukamilika.

Pia ni wigo mwingine anaosema ulimpa furaha ya namna kasi ya ujenzi wa hospitali hiyo na hivyo akaahidi kuipa kipaumbele zaidi katika kupeleka vifaa tiba na watumishi itakapokamilika.

### ALIKOCHANGIA JPM

Waziri Jafo, alitembelea Kituo cha Afya cha Isongole katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, ambacho kilianza kujengwa na wananchi kabla ya Rais Dk. John Magufuli kuchangia Sh. milioni 30 kwa ajili ya ukamilishaji.

Waziri Jafo, ambaye aliwasilisha mchango huo wa Rais, alitembelea kwa lengo la kukagua utekelezaji wa maagizo yake mkuu wa nchi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, anakokiri pia maelekezo yote yalitekelezwa na hadi sasa kituo kimeshafunguliwa.

Aliwapongeza wananchi kwa juhudi zao za kujenga kituo na halmashauri kutekeleza maelekezo husika kwa wakati na aliwataka wananchi wa kata zingine zisizo na vituo vya afya, kuiga staili ya kujitolea, iliyofanywa na wananchi wa Kata ya Isongole.

### WILAYANI CHUNYA

Katika ziara hiyo, pia Waziri Jafo alitembelea Kituo cha Afya cha Chalangwa wilayani Chunya, ambacho ni miongoni mwa vituo 14 vilivyojengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na wananchi, kupitia mfumo wa 'Force Account.'

Taarifa ya wilaya hiyo inaeleza kuwa, serikali ilitoa fedha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi na wananchi walichangia nguvu zao kwa zaidi ya Sh. milioni 60.

Waziri Jafo, kwa mara nyingine alionyesha furaha yake tena kwa tabasamu itokanayo na kituo hicho kilivyojengwa kwa viwango na uzingatiaji wa thamani ya fedha zilizotolewa, akikisifu kwamba ni kizuri, kikubwa kuliko hata baadhi ya hospitali.

Jafo anainisha sifa za ramani na muundo wa kuunganisha idara mbalimbali za kituo hicho zilivyotengenezwa, ikiwa ni pamoja na kuzingatia mahitaji ya watu wa aina zote, wakiwamo wenye ulemavu.

"Kituo hiki ni kizuri sana na ni kikubwa kuliko hospitali za baadhi ya wilaya ikiwamo Wilaya ya Misungwi kule Mwanza. Sasa najua changamoto zenu ikiwamo ya uhaba wa watumishi, tutaishughulikia ndani ya muda mfupi," anasema Waziri Jafo.

Baada ya kukagua Kituo cha Afya cha Chalangwa, Waziri Jafo alitembelea Hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya kukagua hali ya majengo na akazungumza na watumishi kuhusu ahadi ya Rais Dk. Magufuli ya kutoa pesa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuikarabati.

Akiwa hospitalini hapo, alibaini baadhi ya majengo yamechakaa na alipewa historoa kwamba, hospitali hiyo kwa asili ilikuwa ni kituo cha afya kilichopandishwa hadhi, wilaya hiyo inaanzishwa.

Katika kauli ya majumuishi, anaiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, iimarishe huduma zingine katika hospitali hiyo, ikiwamo huduma ya maji yatakayopatikana kwa mfumo wa kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi, kwa ajili ya matumizi wakati wa kiangazi.

Viongozi wa Mkoa Mbeya, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Chalamila, walimwomba Waziri Jafo, uwezekano wa wilaya hiyo kupatiwa fedha kwa ajili ya kujenga hospitali mpya na hiyo iliyopo, iendelee katika nafasi ya kituo cha afya. Chalamila anasema, wilaya ni kongwe na ina idadi kubwa ya watu kwa sasa, tofauti na ilivyokuwa awali ilipoanzishwa, hivyo kwa sasa haikidhi mahitaji.

"Wilaya hii ina kanda kuu mbili, ambazo ni ukanda wa kilimo na ukanda wa madini. Sasa ina ongezeko kubwa la watu kiasi kwamba hospitali hii ya wilaya haikidhi mahitaji. Tunaomba kama inawezekana nayo ipewe Sh. bilioni 1.5 kama zingine, ili wajenge hospitali mpya," aliomba Chalamila.

### RC AWATETEA

Mkuu wa Mkoa anafafanua kwamba, Chunya haina shida ya eneo la ujenzi, hivyo wakipewa fedha wanaweza wakajenga hospitali kubwa na nzuri.

Kutokana na maelezo hayo, Waziri Jafo alikubali kuwa eneo la hospitali hiyo ambalo ni hekta tano pekee halitoshi kwa hospitali ya wilaya na hata baadhi ya majengo, likiwamo la wagonjwa wa nje (OPD) ni ya zamani na yamechakaa, hivyo atalifanyia kazi ombi hilo.

Jafo anasema, wakati anaendelea kulishughulikia suala hilo, pia anaendelea na utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza ahadi ya Rais ya kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya hospitali hiyo na zingine Sh. milioni 200 za Kituo cha Afya cha Makongolosi.

> Kituo hiki ni kizuri sana na ni kikubwa kuliko hospitali za baadhi ya wilaya ikiwamo Wilaya ya Misungwi kule Mwanza. Sasa najua changamoto zenu ikiwamo ya uhaba wa watumishi, tutaishughulikia ndani ya muda mfupi.

### AKUTA UFISADI

Kituo cha Afya cha Mtande kilichopo zaidi ya kilomita 90 kutoka mjini Chunya Mjini, ndicho katika mzunguko wa ziara kinatengeneza historia aina yake mkoa Mbeya, kwa ujenzi wake kugubikwa na ufisadi mkubwa ambao umeikera serikali.

Kwa mujibu wa Taarifa za Wilaya, serikali ilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho na wananchi walichangia nguvu zao kwenye ujenzi, wakishiriki kuchimba msingi, kubeba mawe, kusogeza tofali na hata kuwasaidia mafundi.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alibaini kuwa ujenzi wa kituo hicho unanuka ufisadi ikiwamo kuchakachua baadhi ya vifaa na hivyo akalazimika kuunda tume maalumu kwa ajili ya kuchunguza ili wahusika wachukuliwe hatua.

Taarifa za ufisadi huo iliyowasilishwa kwa Waziri Jafo aliagiza mamlaka zinazohusika, likiwamo Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuchukua hatua za kisheria kubaini ufisadi huo na wahusika wake, baada ya tume kumaliza kazi.

Jafi aling'aka kwamba, serikali haiwezi kuvumilia fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kisha zinapotea katika mikono ya wachache, huku kundi kubwa la wananchi linaendelea kupata shida.

"Nakupongeza Mkuu wa Mkoa kwa kuunda tume. Mimi nilitaka kuunda tume nyingine ya wizara, lakini naamini tume yako itatuletea matokeo mazuri na wahusika wote washughulikiwe kwa mujibu wa sheria," alifafanua Waziri Jafo.

Inaelezwa na wataalamu wa afya, kwamba baadhi ya vituo vya afya vilivyojengwa kwa mfumo wa 'Force Account,' ikiwemo kituo cha kwanza cha mfano cha Ikuti wilayani Rungwe, Ipinda wilayani Kyela na Ikukwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, vina hadhi sawa na hospitali za wilaya, isipokuwa zinakosa baadhi ya vipimo.

AFYA

# Bajeti Lishe Kagera bado shida



Mtoto Safina Ahmad (4) akiendelea kunywa uji wa lishe, katika Tamasha la Mtoto Mwerevu, Wilaya ya Missenyi.

INATOKA UK.17

kijani, labda watoto wawili ambao wazazi wao wameshindwa kufuata maelekezo wanayopewa ndiyo wamebaki katika rangi ya kijivu, lakini tunaendelea kuwahudumia ili nao afya zao ziimarike," anasema.

**MRATIBU LISHE**

Zainath Hassan ni mratibu wa lishe Wilaya ya Missenyi ambaye anasema mwaka 2018/2019 zilitengwa shilingi milioni 38 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za lishe kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, lakini zilizitolewa ni Sh. milioni 5.3.

Anasema, kutokana na kutokutolewa kwa fedha hizo kama ilivyopangwa, baadhi ya shughuli hazikutekelezwa zikiwamo za uchunguzi wa hali ya lishe kwa watoto, ununuzi wa chakula dawa, kufanya uchunguzi wa kuwapo kwa madini joto katika chumvi inayotumika majumbani na kutoa elimu kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Anataja shughuli zilizofanyika kwa kutumia sehemu ndogo ya bajeti iliyotolewa na halmashauri kwa kushirikiana na wafadhili kuwa ni kuzijengea uwezo kamati za maendeleo za kata kadhaa.

Zainath anasema, kikwazo cha kutokutolewa fedha hizo kinakwamisha, huku akitaja ni mapato kidogo ya halmashauri, halmashauri kukosa vipaumbele vingi.

Anawataja wahisani wanaowasaidia ni serikali ya Uingereza kupitia Shirika la IMA World Health chini ya mradi wa Mtoto Mwerevu waliotoa shilingi milioni 67 katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Wengine ni USAID Boresha Afya,

> **Pia wameshirikiana na wadau wa Boresha Afya kwa watoto wenye utapiamlo mkali, na kuwa sasa kuna vituo maalumu 12 ambavyo vinawahudumia watoto hao.**

World Vision, shirika linaloshughulika na masuala ya Ukimwi, utunzaji wa mazingira na lishe la MAPEC na Kikukwe KCDI, wanaotekeleza shughuli zao bila kuingiza fedha katika akaunti ya halmashauri.

Anataja baadhi ya shughuli za lishe zinazotekelezwa na wafadhili hao kuwa ni kubadili tabia katika unyonyeshaji, chakula cha nyongeza kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 24, ushiriki wa wanaume katika malezi ya watoto, usafi na unawaji wa mikono, matendo changamshi na kuwezesha posho kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Nyingine ni kuwezesha vikao vya kamati ya jamii, kuwezesha ufuatiliaji ngazi ya jamii na vituo vya kutolewa huduma za afya na wahudumu wa huduma za mkoba ambao pia hufundisha jinsi ya kuchanganya chakula cha lishe kwa watoto.

Anasema pia kuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imetenga shilingi milioni 42 na katika kipindi cha Julai hadi Desemba zilizokwisha kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za lishe ni shilingi milioni mbili.

"Mkurugenzi ameahidi kutoa pesa zote zilizotengwa katika mwaka huu wa fedha, lakini kwa sasa tumeanza kutumia za wafadhili na baadaye katika nusu ya mwaka wa fedha iliyobaki tutaanza kutumia za bajeti yetu," anasema.

"Pia tulipata shilingi milioni tisa kutoka Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) ambazo utekelezaji wake ulianza Oktoba hadi Desemba mwaka huu, na tayari tumekwishapokea shilingi milioni tatu kwa ajili ya kazi za kutambua maduka yote yanayouza chumvi," anasema.

Baada ya kutambua maduka hayo, fedha hizo za Unicef pia zimetumika kufanya uchunguzi wa kuwapo kwa madini joto katika chumvi inayouzwa madukani.

**VIKWAZO**

Zainath anataja changamoto wanazokabiliana nazo katika utekelezaji shughuli za lishe mbali na kuwa ufinyu wa bajeti, ni uhaba wa vitendea kazi kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii na uelewa mdogo wa jamii kwenye masuala ya lishe.

Anataja changamoto nyingine kuwa ni wananchi wengi kuhangaika na masuala ya kiuchumi na kusahau kuhudumia watoto na kukosa chakula na baadhi ya dawa.

Anatumia fursa hiyo kuitaka jamii kuelewa lishe ni suala mtambuka na kuwa ni jukumu la kila mtu kutoa kipaumbele katika mapambano yake.

"Madhara ya udumavu unaotokana na utapiamlo hayarekebishiki, tunapaswa kuendelea kuelimisha watu waweke katika afya za watoto wao, maana inayoathirika si kaya tu bali halmashauri, mkoa na taifa kwa ujumla," anasema.

Shirika la IMA World Health ambalo mradi wake wa Mtoto Mwerevu unaotekelezwa katika halmashauri zote mkoani Kagera unafikia kikomo tarehe 31 mwaka huu, na limetoa zaidi ya shilingi milioni 400 kwa halmashauri hizo katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba mwaka huu.

**SISTA ISHENGOMA**

Sista Margaret Ishengoma, mtaalamu mabadiliko ya tabia katika lishe kutoka shirika la IMA World Health kupitia mradi wa Mtoto Mwerevu mkoani Kagera, anasema mradi unalenga kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto.

"Tunashirikiana na serikali kwa kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wanakwenda kwenye nyumba za walengwa wetu ambao ni wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili, kuangalia hali ikoje, kuhimiza na kujadiliana ni kitu gani wanaweza kufanya ili kupunguza udumavu kwa watoto," anasema.

Anasema kuwa katika vijiji wanapima watoto na wanapobaini kuna tatizo hilo kwa asilimia 30 wanakaa na kinamama kwa siku 12 wakiwafundisha kwa muda wa kati ya saa mbili hadi matatu kwa siku, katika eneo walilolichagua, ikiwamo darasa la kupika.

"Baada ya siku 12 kambini, tunawapima tena watoto, na cha kushangaza chakula hiki kinatenda maajabu, watoto uzito unaongezeka hata kwa kilo mbili katika kipindi hicho na kuwashangaza wazazi," anasema.

Mradi wa Mtoto Mwerevu ulianza mwaka 2016 kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza, ikitoa ruzuku wajibifu kwa halmashauri ili ziweze kutekeleza shughuli za lishe ambazo zitasaidia kupunguza udumavu kwa watoto.

"Bado tatizo ni kubwa, kwa asilimia ni mkoa wa tisa kitaifa, lakini ukiangalia takwimu ni mkoa wa kwanza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto waliodumaa ambao ni 224,634, na hii ni kutokana na Kagera kuwa na idadi kubwa ya watu," anasema.

Anataja shughuli zilizofanyika na kuwezesha kiwango cha udumavu Kagera kushuka kuwa ni kushirikiana na wadau kutoa elimu kwa kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kutoa elimu katika vituo vya kutolea huduma za afya na kupitia vyombo vya habari.

Anasema, pia wameshirikiana na wadau wa Boresha Afya kwa watoto wenye utapiamlo mkali, na kuwa sasa kuna vituo maalumu 12 ambavyo vinawahudumia watoto hao.

Ofisa lishe huyo, anataja sababu kubwa inayochangia Kagera kuwa na watoto wengi waliodumaa wakati vipo vyakula vya kutosha kuwa, ni ulishaji watoto usiozingatia mlo kamili.

Anataja makundi matano ya vyakula ambavyo wananchi wanapaswa kuwalisha watoto wao kuwa la kwanza ni nafaka, mizizi na ndizi kwa ajili ya kuwapatia wanga, la pili ni vyakula vya wanyama na jamii ya mikunde, la tatu mboga za majani, la nne ni matunda na la tano ni asali, sukari na mafuta.

Kwa mujibu wa utafiti wa TNNS wa mwaka 2018 ulishaji wa chakula cha mtoto Kagera ni asilimia 19.6



# Viwanda mpunga vyalalamikia mita za umeme

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAMILIKI wa viwanda vya kusindika mpunga wilayani Mbarali wamelalamikia mita za umeme wanazofungiwa na Shirika la Umeme (Tanesco) wakidai zinasababisha gharama za uendeshaji wa viwanda hivyo kuwa kubwa kuliko faida wanaoipata.

Akisoma risala ya wamiliki hao kwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, Katibu wa Chama cha wa Miliki wa Viwanda vya Kusindika Mpunga, Mambela Juma, alisema licha ya viwanda hivyo kufanana karibu kwa kila kitu, lakini Tanesco imekuwa ikiwafungia mita za umeme zinazotofautiana.

Alisema baadhi ya mita hizo zinaonyesha matumizi makubwa ya umeme ukilinganisha na baadhi ya mita, hali ambayo inasababisha baadhi ya wamiliki kushindwa kumudu gharama za matumizi ya umeme kwenye viwanda vyao.

Alisema kuwa mbali na tatizo hilo, pia wanakabiliana na tatizo lingine la umeme kukatika ovyo na wakati mwingine kusababisha uharibifu wa mitambo ya viwanda vyao.

Alisema tatizo hilo la umeme kukatika linakwenda sambamba na nyakati nyingine umeme kukosa nguvu ya kuendesha viwanda na hivyo kuwalazimu kusimamisha uzalishaji kusubiri utengamae. Mambila alimwomba Naibu Waziri kuwasaidia kuishinikiza Tanesco kubadilisha transfoma zilizowekwa kwenye maeneo ya viwanda vyao na kuletewa zenye nguvu zaidi ili kuepuka tatizo la umeme kukosa nguvu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema ofisi yake imeshawasiliana na Tanesco kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya miundombinu ya umeme kwenye maeneo ya viwanda ili kuondoa matatizo yanayowakabili wamiliki wa viwanda hivyo.

Alisema viwanda hivyo ni muhimu kwa uchumi wa wilaya yake na nchi kwa ujumla, hivyo ni lazima wahakikishe vinafanya kazi kwa ufanisi muda wote badala ya muda mwingine kufungwa

"Changamoto za wamiliki wa viwanda hivi ofisi yangu inazitambua, na nimeshaanza kuchukua hatua kwa kuwasiliana na Tanesco ambao tumeshakubaliana kwamba waanze kuboresha miundombinu kwenye maeneo haya," alisema Mfune.

Akijibu malalamiko hayo, Manyanya alisema tatizo la viwango vya matumizi ya umeme linasababishwa na mambo mengi ikiwamo namna ya wamiliki wa viwanda wanavyowasha viwanda vyao. Alisema kama kiwanda kina mashine zaidi ya tatu na zote zinawashwa kwa wakati mmoja, ni lazima matumizi ya umeme yaonekane ni makubwa kuliko kawaida kwa sababu mashine zote zinatumia umeme kwa mwingi kwa wakati mmoja wakati zinapowashwa.

Aliwaasa wamiliki hao kubadili mfumo wao kuwasha viwanda vyao kwa kufuata utaratibu na wakati mwingine kuepuka kuwasha mashine ambazo kwa wakati huo huwa hazitumiki.

"Ikiwa una mashine tatu ndani ya kiwanda, usifike ukaziwasha zote kwa wakati mmoja, nakushauri uwashe mashine moja ikishawaka na kuchanganya ndipo unawasha nyingine na yenyewe ikitulia unawasha ya tatu, hii itakusaidia kupunguza matumizi ya umeme badala ya kuwasha zote kwa wakati mmoja," alisema Manyanya.

Kuhusu changamoto ya umeme kukatika na kukosa nguvu, Manyanya aliitaka Tanesco kulishughulikia haraka kwa kubadili transfoma za viwanda hivyo na kuwawekea zenye nguvu zaidi.

Manyanya alisema hilo ni jukumu la Tanesco, na kamwe wamiliki wa viwanda wasihusishwe kwenye gharama hizo za kubadilisha transfoma kwa sababu Rais John Magufuli alishapiga marufuku kuwatoza wamiliki wa viwanda gharama za aina hiyo.



Daladala likikwepa shimo kwenye barabara inayoelekea katikati ya Jiji la Mbeya, katika eneo la njia panda ya Chunya juzi. Shimo hilo, linasababisha baadhi ya wenye magari kuikwepa njia hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Washauriwa kufuatilia michango mifuko hifadhi

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WATUMISHI wametakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia kwa ukaribu michango yao katika mifuko ya hifadhi za jamii ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza wanapostaafu au kupata matatizo kazini.

Wito huo ulitolewa jana na mmoja wa wazee wastaafu, Zabron Henry aliyekutwa nje ya ofisi za mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mzee huyo alibainisha kuwa wengi wa watumishi hawana utamaduni wa kufuatilia michango yao katika mifuko mbalimbali ya hifadhi za jamii ikiwamo ya PSSSF na NSSF.

"Unajua kumekuwapo na kasumba ya baadhi ya watumishi wengi nchi kutokuwa na utamaduni wa kufuatilia michango yao katika mifuko ya hifadhi za jamii na hivyo kupelekea kuibua usumbufu wakati watumishi hao wanapostaafu au kupata matatizo kazini," alisema Zabron.

Alisema mifuko ya hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma ipo kwa ajili ya watumishi wote, hivyo kila mtumishi ana haki ya kufuatilia michango yake.

Alisema tangu kuanzishwa kwa ofisi ya PSSSF mkoa wa Mbeya, imekuwa msaada mkubwa kwa watumishi pamoja na wastaafu ambao wamekuwa wakifika katika ofisi hizo kupata huduma.

"Tangu mifuko kuunganishwa na kuwa mfuko wa PSSSF kumekuwa na maboresho mazuri ya huduma ambazo zinazingatia muda na umakini wa kazi, na tunaipongeza serikali kwa kuanzisha mfumo huu," alisema.

Jitihada za kumpata Meneja wa PSSSF kwa Mkoa wa Mbeya kuzungumzia jitihada zinazofanywa na mfuko kwa lengo la kuboresha huduma za wateja zinaendelea, kutokana na kutafutwa mara kadhaa bila mafanikio.

Muundo wa mfuko wa PSSSF unajumuisha mifuko minne ya pensheni ambayo ni PSPF, LAPF, PPF na GEPF ambapo waliokuwa wanachama wa mifuko hiyo wakiwamo watumishi, wastaafu na warithi waliopo katika mifuko walihamishiwa PSSSF.

# Rungwe yakamilisha ujenzi wa madarasa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WILAYA ya Rungwe, imekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa sita vilivyokuwa vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi 240 waliofaulu mitihani ya darasa la saba mwaka jana, lakini majina yao yamezuiliwa kusubiri kukamilika kwa vyumba hivyo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Chalya, alipokuwa anatoa taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo ambapo alisema wilaya iko tayari wanafunzi wote waliofaulu kuanza masomo.

Alisema wilaya yake yenye halmashauri mbili za Rungwe na Busokelo, vyumba vyote vilivyokuwa vinahitajika vilikuwa katika Halmashauri ya Rungwe.

Chalya alisema vyumba hivyo vimekamilika mapema kutokana na ushirikiano mzuri baina ya wananchi na viongozi wa halmashauri hiyo ambao walishirikiana kwa ukaribu kuhakikisha watoto wanaanza masomo mapema. Alisema Halmashauri ya Busokelo haikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa, na kwamba wanafunzi wote waliofaulu walikuwa wameshapangiwa shule na sasa wanaendelea na maandalizi ya mwakani.

"Nawashukuru viongozi wenzangu kwa ushirikiano katika kukamilisha vyumba hivi, kwa sasa hatuna deni, lakini tunaendelea na mapambano kwa ajili ya maandalizi ya mwakani, hatuhitaji tuje tuwe na tatizo tena," alisema Chalya.

Aliwataka wazazi waendelee kushirikiana na serikali kuhakikisha miundombinu ya shule zao inaboreka ili kuinua kiwango cha elimu katika wilaya hiyo.

Hivi karibuni Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Jeremiah Minja, aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kukamilisha vyumba vya madarasa kabla ya Januari 15, mwaka huu, ili wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya darasa la saba waanze masomo mapema.

Taarifa ya mkoa inaonyesha kuwa mkoa huo ulikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 59 ambavyo vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi 2,716 waliokosa nafasi.



# Jafo aonya wanaozuia wanafunzi kuandikishwa kisa cheti kuzaliwa

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema ni marufuku mwanafunzi kuzuiwa kuandikishwa darasa la kwanza kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa.

Jafo alitoa onyo hilo alipozuru wilayani Bahi kukagua uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa shule za msingi na mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari.

Alisema amepokea malalamiko kutoka baadhi ya maeneo kuwa wanafunzi wa darasa la kwanza hawaandikishwi kama hawana vyeti vya kuzaliwa.

"Nimeona nitoe ufafanuzi kuhusu suala hili kuwa cheti cha kuzaliwa ni haki ya kila mtoto, lakini kisimzuie mtoto huyo kuanza shule eti kwa sababu tu hajakipata. "Watoto wote wapokewe, waandikishwe na waanze masomo huku wazazi wao wakiendelea na mchakato wa kuwatafutia vyeti hivyo," aliagiza.

Alisema hataki kusikia eneo lolote mtoto ameachwa kupokewa shuleni kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa, lakini kila mzazi ahakikishe ndani ya miezi minne, anapata cheti hicho wakati mtoto akiendelea na masomo.


Akizungumza wakati akikagua mapokezi ya kidato cha kwanza, Jafo alisema wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti katika muda uliopangwa na wapokewe bila masharti ya michango ya unga, mahindi au maharage.

Alisema serikali inatoa elimu msingi bila malipo, hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kupata elimu bila bugudha ya aina yoyote. Waziri Jafo aliupongeza uongozi wa Wilaya ya Bahi kwa umakini walioonyesha katika uandikishaji wa darasa la kwanza na maandalizi mazuri katika mapokezi ya kidato cha kwanza pamoja na usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani huko.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema walishafanya kampeni ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, hivyo watoto wengi wanaonza shule hivi sasa wanavyo.

Alibainisha kuwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Wilaya ya Bahi ni 2,712 na kikwazo kilichopo ni uhaba wa madawati, ambao alidai unafanyiwa kazi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkakatika, John Laurent, alisema shule yake ina malengo ya kuandikisha wanafunzi 180 na kwa siku ya kwanza tu ya kufungua, waliandikisha wanafunzi 134. "Wanafunzi wote walioletwa shuleni kwetu tumewaandikisha na endapo mtoto hana cheti cha kuzaliwa, tulitumia kadi la kliniki kupata taarifa sahihi za mtoto na hatujarudisha mwanafunzi hata mmoja, wote wamepokewa na wameanza masomo," alidai.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 500 kama gawio la serikali kutoka kwa Mkuu Kitengo cha Fedha Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Priscilla Mushi (kulia) na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Mipango, Utawala na Fedha, Prof. Donald Mpanduji (kushoto), katika hafla iliyofanyika jijini humo jana. Katikati ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji na Msajili wa Hazina, Athuman Mbutuka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TCRA yatoa neno usajili laini simu alama vidole

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) Kanda ya Kati, imewataka wananchi wa mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma na Dodoma kutumia muda uliongezwa na Rais John Magufuli kusajili laini zao za simu kwa alama za vidole, ili wazitumie kwa ufasaha katika kufanya maendeleo.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Kati, Antonia Manyanda, alitoa rai hiyo alipozungumzia mwitikio wa wakazi wa kanda hiyo kusajili laini zao za simu zikiwa zimebaki siku 11 kabla ya kufungwa kwa usajili huo. "Nawaomba wananchi waendelee kujitokeza kusajili laini zao kwa sababu teknolojia ya simu inakua kila kukicha na simu za mkononi ni ofisi ya mkononi, hivyo ni vyema watu wasajili," alihimiza.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 31 mwaka jana, asilimia 50 ya laini za simu katika eneo hilo zilikuwa zimesajiliwa na mfumo huo wa kisasa.

Alisema TCRA inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kusajili laini za simu kwa mfumo huo hususani kipindi hiki ambacho teknolojia inakua kila kukicha.

Alisema watu wakisajili laini za simu, itawarahisishia kufanya vitu vya maendeleo kupitia simu zao za kiganjani ambazo zitakuwa zimesajiliwa.

"Tutaendelea kutoa elimu kila sehemu kwa sababu tunahitaji kuona wananchi wanakuwa na uelewa juu ya kusajili laini za simu za mkononi," alisema.

Manyanda alisema hakuna sababu ya watu kuzembea kampeni hiyo ya usajili kwa kuwa lengo ni kuhakikisha kila mwenye laini ya simu anaisajili kwa mfumo huo, vinginevyo itafungwa.

# Waokoa mamilioni 11 wakipandikizwa figo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TANGU kuanza kwa huduma ya upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), wagonjwa 11 wamepatiwa huduma hiyo huku mamilioni ya shilingi yakiokolewa, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana kuwa upandikizaji wa figo kwa mgonjwa unagharimu kati ya Sh. milioni 22 na 25, lakini gharama za matibabu hayo nje ya nchi ni zaidi ya Sh. milioni 100 kwa kila mgonjwa.

Dk. Chandika aliyasema hayo baada ya kupandikizwa wagonjwa wengine wanne, akieleza kuwa kutolewa kwa huduma hiyo katika hospitali hiyo, kumeokoa fedha nyingi ambazo zilikuwa zikitumika kutibu wagonjwa nje ya nchi, hasa India.

Alisema gharama inayotumika kwa mgonjwa nje ya nchi inatosha kuhudumia wagonjwa watano katika hospitali hiyo na kwamba kwa wagonjwa saba wa awali, ziliokolewa Sh. milioni 700.

"Tumeweza kuipunguzia serikali gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa ajili ya kupandikizwa figo, na katika wagonjwa wale saba wa awali, hakuna mgonjwa hata mmoja aliyepoteza maisha, wanaendelea vizuri na shughuli zao," alitamba.

Alisema upandikizaji huo ulikuwa ukifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wataalamu kutoka Tokushukay Medical Corporation ya Japan ambao baada ya upandikizaji huo wa watu wanne, ni mwisho kwao kuja nchi kutoa huduma hiyo kutokana na madaktari wa ndani kukomaa kwenye utoaji huduma hiyo.

"Huu upandikizaji uliofanyika kwa wagonjwa wanne, ulianza Januari 6, mwaka huu na umefanyika kwa umakini na tumepata mafanikio makubwa.

"Tunashukuru Japan, wao walilenga kutoa ujuzi kwa wataalamu wetu wa Kitanzania, na baada ya kuona wamekomaa, kwa sasa hawatakuja, huduma hii itafanywa na Watanzania," alisema.

Dk. Chandika alisema hospitali hiyo na wataalamu wake wako tayari kutoa huduma bora ya upandikizaji kutokana na ujuzi walioupata kutoka Japan.

"Tuna madaktari wanne ambao wamepata mafunzo kuhusu upandikizaji figo, hawa wameenda Japan mara mbili, siyo kwenda kuangalia, bali kushiriki kabisa kwenye upasuaji na upandikizaji maana kule wenzetu wanafanya mara kwa mara," alisema.

Alieleza kuwa wataalamu hao wa nje wataitwa au kuombwa ushauri kama itatokea mmoja wa wagonjwa ana shida ambayo si ya kawaida.

Mwenyekiti wa jopo la wataalamu kutoka Japan, Prof. Kobayashi Shuzo, alipongeza Tanzania kwa kuimarisha huduma za kibingwa ikiwamo upandikizaji figo na kwamba hospitali hiyo mbali na kutoa huduma kwa Watanzania, itatibu watu wa mataifa mengine.

Mmoja wa wanufaika wa huduma hiyo, Leah Nkonoki, alisema tangu amepandikizwa figo mwaka 2018, hajawahi kuumwa ugonjwa wowote na anaendelea na shughuli zake.

Alisema alipewa figo na dada yake ambaye naye anaendelea vyema.

"Awali nilikuwa nimedhoofu sana, lakini kwa sasa naendelea vizuri, sisi sote tuliofanyiwa awali tulikuja jana (juzi) na waliotupima na tunaendelea vizuri, masharti tuliyopewa ni kuepuka kula zabibu, machungwa ili kuepuka kupandisha kinga ya mwili na kuua figo," alisema.





# Ujenzi uwanja ndege kuanza

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, kesho anatarajiwa kuweka jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege huko Nugwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisa uhusiano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Mulhat Yussuf Said, alisema katika hafla hiyo kutakuwa na shughuli mbalimbali ambazo ni muhimu wananchi kufika katika eneo hilo ili kujionea ikiwamo maonyesho ya anga. Alisema maonyesho hayo yatajumuisha michezo ya kuruka kwa kutumia puto (parachute jumping) na Skydiving.

Alisema baadhi ya ndege zitatua katika viwanja hivyo zikitokea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume mjini Unguja.

Aliwataka wananchi na wafanyabiashara wadogo na wakubwa kushiriki katika hafla hiyo ambayo ni fursa nzuri kwao kwa biashara na kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, alieleza kuwa uamuzi wa ZAA wa kujenga uwanja huo huko Nungwi ni matokeo ya ongezeko kubwa la watalii katika ukanda wa Kaskazini Unguja. Alieleza kuwa pia uwanja huo utarahisisha usafiri wa anga kwa watalii na wananchi kwa ujumla kwa kuwa uwanja huo pia utatumika kama ni uwanja mbadala wa Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kusaidia masuala ya ulinzi na kurahisisha utafutaji na uokozi yanapotokea majaga.

Alisema viwanja hivyo vina ukubwa wa kilomita mbili urefu na upana wa mita 200 ambapo unahusisha na jengo la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria 350, ujenzi wa maegesho ya ndege.

"Nitumie fursa hii adhimu kuwakaribisha kwa mara nyingine tena wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika tukio hili muhimu na la kihistoria kwa nchi yetu kwa kuwa linalenga kutuunganisha zaidi sisi wananchi hususan wa kipato cha chini," alisema.

Aliongeza: "Kwa kuwa sasa bila ya shaka gharama za nauli ya ndege zitakuwa na ahuweni kwa kuwa ujenzi huu hautoishia Nungwi pekee yake bali utahusisha ujenzi mwingine wa uwanja wa ndege eneo la Muwambe, Pemba ambapo ni mwendo wa saa chache kutoka Nungwi hadi Muwambe."

# Shein akumbushia Zanzibar ilikopitia kielimu

Na Rahma Suleimaan,
ZANZIBAR

USHAURI umetolewa kuwa wakati Zanzibar ikiadhimishia miaka 56 ya Mapinduzi, ni vyema wananchi wakajua kuwa kabla ya Mapinduzi hayo hapakuwa na usawa, bali palikuwa na mifarakano.

Hayo yalielezwa jana na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la Shule ya Sekondari Ziwakije Wingwi Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema Septemba 23, mwaka 964 Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, alitangaza kuwa elimu itatolewa bure kwa watu wote wa Unguja na Pemba, jambo ambalo na yeye katika awamu yake ya saba anayoiongoza analiendeleza.

Alisema mpaka Mapinduzi yanafanyika, Zanzibar ilikuwa na shule za maandalizi (chekechea) ambazo ni Saateni na Jang'ombe ambapo hivi sasa kuna shule za maandalizi 382.

Aidha, alisema kabla ya Mapinduzi hayo pia kulikuwa na shule za msingi 62, na hivi sasa zipo 381, na kuwa shule za sekondari zilikuwa nne, lakini kwa sasa zipo 2,734. Alieleza kuwa elimu ilianza kutolewa Zanzibar mwaka 1890, ambapo ilikuwa ikitolewa kwa jamii ya Kihindi.

Alisema tangu alipoingia madarakani, juhudi za makusudi amezichukua na kupelea kujenga shule 48 zikiwamo za sekondari na msingi. Alisema serikali imebadilisha mitaala ambapo kabla ya Mapinduzi elimu iliyotolewa mwisho ilikuwa ya darasa la nane kwa watoto wa wanyonge.

Alisema miaka 20 iliyopita Zanzibar haikuwa na chuo kikuu hata kimoja, lakini sasa ina vyuo vikuu vitatu ambavyo vinapokea wanafunzi kutoka ndani na nje ya Zanzibar.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema kuwa jengo hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya

uhaba wa nafasi kwa wanafunzi shuleni.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idriss Muslim Hija, akisoma taarifa ya kitaalamu juu ya ujenzi wa shule hiyo alisema kuwa shule hiyo ina pacha wake ambayo ni shule ya Mwanakwerekwe ambayo itawekwa jiwe la msingi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Konde, wakiimba wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la Shule ya Sekondari ya Wingwi, Wilaya ya Micheweni Pemba, juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho za Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Balozi Karume aona fursa nyingine utalii

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Ali Karume, ameushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kuyafanyia matengenezo maeneo ya kihistoria ili yawe kivutio cha utalii.

Alisema kwa muda mrefu maeneo ya kihistoria yalikosa kufanyiwa ukarabati na kupelekea kuikosesha serikali mapato.

Akizungumza katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi vyumba ya kihistoria ya Wareno eneo la Fukuchani Mkoa wa Kaskazini Unguja, Balozi

Karume alisema maeneo ya historia yanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa nchi iwapo miondombinu yake itafanyiwa ukarabati na kuwa kivutio cha utalii.

Alisema Serikali ya Dk. Ali Mohamed Shein imeweka mikakati ya kuyafanyia marekebisho maeneo ya kihistoria ili kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini. Aidha, aliwaomba wananchi, taasisi binafsi, shehia na wanafunzi kushirikiana na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale katika kuyalinda na kuyatunza maeneo hayo ili yaweze kuwa endelevu.

Alieleza idara hiyo kuweka utaratibu wa kutangaza katika vyombo vya habari ili wananchi wapate uelewa wa maeneo hayo na kuweza kutekeleza kwa vitendo utalii wa ndani. Balozi Karume aliwakumbusha watendaji wa idara hiyo, kuajiri watu wenye uelewa wa masuala ya kihistoria ili kuepuka ubabaishaji wakati wa kutembeza watalii wanaoingia nchini.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khadija Bakari Juma, alisema wameyafanyia ukarabati zaidi ya maeneo 85 ya kihistoria na wataendelea kuyafanyiwa ukarabati maeneo mengine kadri ya uwezo wa serikali utakaporuhusu.

Alibainisha kuwa ukarabati wa nyumba ya kihistoria ya Wareno Fukuchani umegharimu zaidi ya Sh. milioni 290 zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# Uchafu machinjio wahatarisha afya walaji

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAFANYABIASHARA wanaochinja nyama katika machinjio ya Tunduru, wamelalamikia uduni wa miundombinu hiyo, hivyo kuiomba serikali kuyaboresha na kuwafanya walaji kupata kitoweo bora.

Hayo yalisemwa juzi na wafanyabiashara wanaochinja ng'ombe na mbuzi katika machinjio hayo, huku wakisema hivi sasa yana hali mbaya ikilinganishwa na huduma inayotolewa katika eneo hilo.

Hashim Issa, Issa Mohamedi na Yasini Abdalah walisema kwa nyakati tofauti kuwa takriban miaka miwili, machinjio hayo hayana maji hali ambayo imekuwa ikiwafanya wachinjaji kuosha nyama kwa kutumia maji yanayotoka katika vidimbwi.

Walisema mbali na kutokuwapo kwa huduma hiyo, pia watu wanaokwenda kuchinja mifugo yao wamekuwa wakijisaidia porini katika kipindi chote hicho na kuhatarisha afya za walaji wa kitoweo na wafanyakazi wa eneo hilo.

Kwa mujibu wa watu hao, vyoo vipo lakini kutokana na kutokuwapo kwa huduma ya maji, hivyo vimefungwa na kusababisha ugumu wa kupata huduma hiyo kwa wateja wao.

Akizungumza kwa niaba ya vibarua walioajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa ajili ya kufanya usafi katika eneo hilo, Bakari Hashim, pamoja na kukiri kukithiri kwa uchafu ndani na nje ya machinjio hayo, alisema chanzo ni mwajiri wao kutowalipa stahiki zao kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu sasa.

Hashim alisema hata usafi ambao wamekuwa wakiufanya ndani hutokana na posho au nyama kidogo ambayo hupewa na wachinjaji kama motisha kwa kazi hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wakifanya usafi wa ndani ya machinjio pekee na kwenda kufanya vibarua vingine ili kumudu kuhudumia familia zao.

"Kutolipwa stahiki zetu kwa muda mrefu kumekuwa kikwazo cha sisi kuendelea na shughuli za kusafisha maeneo yote ya machinjo," alisema Hashim.

Hata alipokutwa akikagua nyama bila kuvaa sare, msimamizi na mkaguzi wa nyama katika machinjio hayo, Dk. Fredy Mushi, alisema alivua sare kwa ajili ya kwenda kufutilia maji katika mabomba aliyodai kuingizwa wiki moja iliyopita.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gasper Balyomi, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kwamba tayari halmashauri yake imetenga fedha kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya kufanya ukarabati.

"Ni kweli tatizo hilo lipo na tayari tumekwishatenga Sh. milioni nne kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika machinjio yetu," alisisitiza Balyomi.

Akizungumzia mgomo wa vibarua wanaofanya usafi katika machinjio hayo, alisema tatizo lilitokana na idara husika kutoweka kifungu ambacho kingetumika kuwalipa posho zao.

Alisema baada ya kuliona hilo, tayari amekwishaandaa utaratibu mwingine wa kuanza kuwalipa vibarua hao ili kuondoa malalamiko yaliyodumu muda mrefu.



Mfanyabiashara wa ukwaju katika Soko la Temeke Dar es Salaam, Bakari Mkumba, akiuandaa kwa ajili ya kuwauzia wateja sokoni hapo, jana, ambapo kilo moja iliuzwa kwa bei ya 2,500/-. Mkumba alisema asilimia kubwa ya wateja wake ni wajasiriamali wanaotengeneza juisi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafanyabiashara wa nishati wapewa onyo

**Na Neema Emmanuel,**

WAFANYABIASHARA wa nishati na mafuta wametakiwa kuwalinda wateja wao kwa kufuata, kuzingatia sheria na kutokuchezea vipimo hivyo kwa lengo la kuwaibia wateja.

Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mwanza, Albogast Kajungu, alisema hayo juzi katika kikao kazi cha utoaji elimu ya uzingatiaji sheria katika biashara ya nishati kwa wamiliki wa vituo vya mafuta jijini hapa.

Alisema WMA inafanya jitihada za kupunguza kero kwa wadau wake kwa kutoa elimu ya vipimo, hivyo hawatawafumbia macho wafanyabiashara ambao watawaibia wateja kwa njia ya vipimo.

Kajungu alisema taasisi ya kusimamia masuala ya vipimo nchini ilikuwapo kabla ya uhuru mwaka 1961 na ilianzishwa kwa lengo la kuilinda jamii dhidi ya madhara yatokanayo na matumizi ya vipimo visiyo sahihi katika biashara na huduma za jamii.

Kutokana na ukweli huo, meneja huyo alionya kuwa mfanyabiashara atakayekwenda kinyume, sheria itachukua mkondo wake.

Sambamba na hayo, aliwataka wafanyabiashara kutumia fursa ya uwapo wa kituo cha upimaji uwezo wa matangi ya magari ya kubebea mafuta kilichoko Nyamongoro na kuondokana na adha ya kutumia gharama na umbali mrefu kuifuata huduma hiyo jijini Dar es Salaam.

"Watu wengi walikuwa hawajui nini kinafanyika hapa kitu ambacho wengi walikiita kituo hiki kuwa ni mizani ya kupima magari kumbe sivyo. Hiki ni kituo maalum na cha kisasa kwa ajili ya kupima matangi ya magari yanayobeba mafuta. Pia tuna uwezo wa kupima magari 16 kwa saa 12 kuanzia asubuhi hadi jioni," alisema Kajungu.

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Christopher Kadio, alitilia maanani suala la sheria ya kumlinda mteja huku akiwataka wafanyabiashara kufuata sheria ili kuleta tija yenye maendeleo.

"Mimi kwenye kutafakari kwangu nimeona kwenye hili zipo sheria nyingi, hivyo kwa sababu ninyi mna wateja na wanahitaji huduma iliyo bora, naona tuanze na hili linalomtilia maanani mteja kwa sababu yeye anahitaji huduma kwenu. Ni vyema tukahakikisha analindwa na sheria hii ndiyo tuipe kipaumbele," alisema Kadio.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Mafuta Tanzania (Tapsoa), Chacha Kenene, alikubaliana na hatua hiyo na kuwaomba wafanyabiashara wenzake kuwa waaminifu na kufuata yale waliyoelekezwa na kuhakikisha pampu zao muda wote zinakuwa kwenye uhalisia wake.

## Vibaka sasa tishio Kahama

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

BAADHI ya wananchi mjini Kahama wameishauri serikali wilayani hapa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi kwa kudhibiti matukio ya uhalifu yanayofanywa na vibaka katika maeneo mbalimbali.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema matukio ya watu kukabwa yamekithiri katika hasa nyakati za usiku jambo ambalo linasababisha hofu kubwa kwa wananchi.

Hashimu Baraka, Seif Mohamed na Abdala Mitimingi wakazi wa Mtaa wa Nyohogo, walisema mitaa ya Nyohogo na Sazia imekithiri kwa matukio haya, huku wakiyataja maeneo mengine kuwa ni Majengo, Igomelo, Shunu na Nyahanga, Malunga.

Kwa mujibu wa watu hao, baadhi ya wananchi wamekuwa wakivamiwa na vibaka nyakati za usiku pindi wanapotoka kwenye shughuli zao.

Mkazi wa Nyahanga, Editha Adriano, ambaye alinusurika kuvamiwa na vibaka akiwa anatoka kazini majira ya saa 2:00 usiku katika Mtaa wa Nyahanga, alisema baada ya vibaka hao kumvamia, alipiga kelele na kwa bahati nzuri wapita njia wakamwokoa na vibaka walikimbia.

Mkazi mwingine wa Nyahanga, Sebastiana Mnakaya, naye alivamiwa na vibaka usiku majira ya saa sita wakati anatoka kazini na kujeruhiwa kwa mapanga na vitu vingine vizito.

Akizungumza hivi karibuni, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna msaidizi (ACP) Deborah Magiligimba, alisema jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi na usalama kwa kufanya doria katika maeneo mbalimbali ili kuwabaini watu wanaojihusisha na uhalifu.

Kamanda Magiligimba alisema wamejipanga kuzunguka maeneo mbalimbali na kuanzisha misako ya mara kwa mara katika ngazi zote ili kuhakikisha wananchi wanakuwa salama.

# HABARI KIMATAIFA

## Abiria 176 wafariki dunia ajali ya ndege

**KYIV,** Ukrain

NDEGE ya Ukraine aina ya Boeing-737 iliyokuwa na abiria zaidi ya 170 imeanguka nchini Iran.

Watoa huduma wa Shirika la Msalaba Mwekundu wa Iran walieleza kuwa hakuna dalili yoyote inayoonyesha endapo kuna mtu aliyepona katika ajali hiyo.

Ndege hiyo yenye namba PS752 inayomilikiwa na Shirika la Kimataifa la Ndege la Ukraine ilianguka muda mfupi baada ya kuanza safari katika Uwanja wa Ndege wa Imam (Khomeini) mjini Tehran.

Taarifa iliyotolewa na ubalozi wa Tehran imesema kuwa injini ya ndege iliharibika na hakuna uhusiano wowote wa kigaidi.

"Kwa mujibu wa taarifa za awali, ndege hiyo ilianguka kwa sababu ya hitilafu za kiufundi. Kwa sasa suala la ndege hiyo kuhusishwa na ugaidi limeondoka," ilieleza taarifa kutoka ubalozi wa Terhan kupitia mtandao wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Ukraine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Vadym Prystaiko, alisema abiria waliokuwamo kwenye ndege hiyo ni raia 82 wa Wairan, 63 Wacanada 11 wa Ukraine pamoja na wafanyakazi, wa Sweden 10, raia wanne wa Afghanistan, watatu wa Uingereza na watatu wa Ujerumani.

Ripoti za awali zinadai kuwa ndege hiyo ilikuwa safarini kuelekea mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Serikali ya Ukraine imesema kuwa inafanya uchunguzi kujua chanzo cha ajali hiyo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa ziara ya Rais Volodymyr Zelensky kuelekea Oman ilisitishwa na amerejea mjini Kyiv.

"Pole zangu nyingi kwa ndugu na jamaa wa abiria wote waliokuwa katika ndege hiyo pamoja na wafanyakazi wa ndege hiyo," alisema Volodymyr.

Haijabainika ikiwa ajali hiyo ina uhusiano wowote na mzozo wa Iran-na Marekani.

Waziri Mkuu Oleksiy Honcharuk alisema abiria wapatao 168 na wafanyakazi tisa wa ndege hiyo wamedhibitishwa kuwapo kwenye ndege hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Ndege la Kimataifa la Ukraine limesitisha safari zake zote za ndege za Tehran. Ndege iliyopata ajali ilifanyiwa matengenezo siku ya Jumatatu.

Kikosi cha uokoaji kimetumwa katika eneo la tukio licha ya kwamba wahudumu wa Msalaba Mwekundu kuvitaarifu vyombo vya habari kuwa haiwezekani kuwa kuna mtu yeyote angeweza kupona katika ajali hiyo.

Kikosi cha uokoaji kimepata moja ya kisanduku cheusi cha ndege hiyo, vyombo vya habari vya Iran vimeripoti.

Ukraine imetuma ndege maalumu kwa ajili ya kurejesha miili ya waliokufa katika ajali hiyo kwa kutegemea maamuzi ya Iran. **BBC**



Wananchi wa Sudan wakiyakimbia makazi yao baada ya kutokea mapigano kati ya Waarabu na wasio Waarabu katika Jimbo la Darfur Magharibi mwa nchi hiyo. **PICHA: ALLIANCE**

# Iran yashambulia vituo vya Marekani

**TEHRAN,** Iran

IRAN imefanya mashambulio ya makombora dhidi ya ngome za kijeshi za Marekani nchini Iraq kama hatua ya kilipiza kisasi mauaji ya Jenerali Qasem Soleimani.

Makombora kadhaa yaliyorushwa kutoka Iran yalilenga eneo la Irbil na Al Asad, magharibi mwa mji wa Baghdad.

Runinga ya kitaifa ya Iran ilieleza kuwa shambulio hilo ni la kulipiza kisasi mauaji ya Jenerali Soleimani aliyeuawa katika shambulio la ndege isiyokuwa na rubani mjini Baghdad, kufuatia agizo la Rais wa Marekani, Donald Trump.

Baada ya shambulio hiyo, Rais Trump jana aliandika katika ukurasa wa akaunti yake ya mtandao wa Twitter yake akisema kwamba: "Mambo ni shwari" na kuongeza kuwa nchi yake kwa sasa inatathmini kiwango cha athari ya mashambulio hayo.

Kambi hizo mbili za kijeshi za nchini Iraq ambayo ni makao ya vikosi vya muungano vinavyoongozwa na Marekani zililengwa- moja ya Al Asad na nyingine mjini Irbil zilishambuliwa saa kadhaa baada ya mazishi ya Soleimani.

Kambi ya Al Asad, ambayo iko mji wa Anbar Magharibi mwa Iraq ilishambuliwa kwa makombola sita.

**Tunawaonya washirika wote wa Marekani ambao wameruhusu vikosi vya Marekani kuwa katika ardhi yao, kwamba wakijaribu uchokozi wa aina yoyote dhidi ya Iran yatalengwa.**

Kiongozi mkuu wa kidini wa Iran, Ayatollah Khamenei alisema shambulio hilo ni kofi la usoni kwa Marekani.

"Tukizungumzia makabiliano ya kijeshi shambulio hili halitoshi, cha msingi kwa sasa ni kuhakikisha uwapo wa kifisadi wa Marekani lazima ufike mwisho," alisema Khamenei.

Hili ndilo shambulio la Iran la moja kwa moja dhidi ya Marekani tangu kutekwa kwa ubalozi wa Marekani mjini Tehran mwaka 1979.

Jeshi la ulinzi la Iran, Revolutionary Guard limesema kuwa shambulio hilo ni la kulipiza kisasi kifo cha Soleimani cha Ijumaa iliyopita, kufuatia agizo la Rais Trump.

"Tunawaonya washirika wote wa Marekani ambao wameruhusu vikosi vya Marekani kuwa katika ardhi yao, kwamba wakijaribu uchokozi wa aina yoyote dhidi ya Iran yatalengwa," ilisema kupitia taarifa yake iliyotolewa na shirika la habari la Iran, IRNA.

Awali, Rais Trump alisema kuwa hatua ya kuondoa vikosi vyake Iraq itakuwa na athari mbaya sana kwa nchi hiyo. Marekani ina wanajeshi wapato 5,000 nchini Iraq.

Wakati huo huo, Waziri wa Ulinzi wa Uingereza, Ben Wallace, alisema nchi yake imechukua hatua ya tahadhari kwa kuweka tayari manuari yake ya kivita na helikopta za kijeshi baada ya kuongezeka kwa hali ya taharuki mashariki ya kati.

Kuuawa kwa Jenerali Soleimani Januari 3, mwaka huu, kulizorotesha uhusiano kati ya Iran na Marekani.

Jenerali Soleimani alikuwa kiongozi wa operesheni ya kijeshi ya Iran katika eneo la mashariki ya kati, lakini serikali ya Marekani ilimuona kuwa gaidi, ambaye alihusika na vifo vya mamia ya wanajeshi wake na kwamba alikuwa akipanga shambulio hatari.

Rais Trump, kwa upande wake, alisema kuwa Marekani itajibu jaribio lolote la kulipiza kisasi pengine kwa njia kali zaidi.

"Alikuwa adui lakini sasa sio adui tena. Amekufa. "Alikuwa anapanga shambulio kubwa, shambulio hatari dhidi yetu. Sidhani mtu yeyote anaweza kulalamika kuhusiana na hilo."

Mamilioni ya raia wa Iran juzi walijitokeza kwenye mazishi ya kamanda huyo wa kijeshi, wakibeba mabango na kupaza sauti wakisema kifo kwa America na kifo kwa Trump. **BBC**

# Waziri aagiza TPC kufanya kazi kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, amelitaka Shirika la Posta (TPC) kufanya kazi kidijitali kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), ili kuendana na kasi ya serikali.

Nditiye alisema jana jijini hapa kuwa kuna haja wafanyakazi wa shirika hilo wafanye kazi kidijitali zaidi kwa kuwa hivi sasa dunia inakwenda kidijitali.

Aliwataka wahakikishe kila mahali nchini kuna ofisi za shirika hilo na watoe huduma kwa kuzingatia matakwa ya wateja wao kwa bidii, uaminifu na ubunifu, akiamini kufanya hivyo kunaongeza mapato ya shirika na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Aliwapongeza wafanyakazi wa shirika hilo na menejimenti yake kwa kujiendesha wenyewe bila kutegemea ruzuku ya serikali na kutoa gawio na mchango kwa serikali kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo.

Pia alisema anawapongeza viongozi na wafanyakazi wa shirika hilo kwa kufanikiwa kuliondoa kwenye orodha ya mashirika yaliyowekwa chini ya uangalizi wa serikali kwa ajili ya kubinafsishwa.

Nditiye aliitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) kukagua mabasi ya abiria yanayosafirisha vifurushi, vipeto na barua bila kuwa na leseni na kufuata utaratibu.

"Hadi sasa, kuna mabasi ya abiria yanasafirisha barua, vifurushi na vipeto, TCRA wakague mabasi hayo asubuhi kama wanavyofanya Latra, na wakiona wamepakia bila leseni, mabasi hayo yachukuliwe hatua mara moja na waache kusafirisha bidhaa hizo mara moja," aliagiza.

Alilitaka shirika hilo kufanya biashara kwa kuwa wakipata wanarudisha gawio serikalini na si kila kitu kisafirishwe na mtu au taasisi binafsi kwa kuwa vitu vingine ni nyeti.

Aliwaomba wananchi kulitumia shirika hilo katika huduma za usafirishaji na mawasiliano kwa kuwa vitu havipotei, akiwashauri waache kusafirisha vitu muhimu kama vyeti vya elimu kwa kutumia taasisi zingine tofauti na shirika hilo.




Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, akizungumza wakati akifungua mkutano wa 26 wa Baraza la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania jijini Dodoma jana. **PICHA: WUUM**

# CCM yahamasisha ujenzi madarasa

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mara, kimewataka viongozi wa ngazi mbalimbali wa chama na serikali kuhamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa ili wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza na wale walioandikishwa kuanza darasa la kwanza, wapate mahali pa kusomea.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Samwel Kiboye, alitoa agizo hilo wakati akitoa salamu za rambirambi kwenye msiba wa Diwani wa Wariku katika Hamashauri ya Mji wa Bunda, Lawi Nyamajeje (CCM).

Kiboye alisema wanafunzi wengi wamechaguliwa kujiunga sekondari pamoja na wanaoandikishwa darasa la kwanza, lakini kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa.

Kutokana na upungufu huo, Kiboye alisema ni jukumu la kila kiongozi wa ngazi mbalimbali kuhamasisha wananchi katika eneo lake kujenga vyumba vya madarasa na kwamba viongozi hao pia wanapaswa kushiriki katika ujenzi huo.

Alisema ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa ni muhimu kwa kuwa visipokamilika kwa wakati, watoto wataendelea kukaa mitaani, hivyo kukosa haki yao ya msingi ya kupata elimu.

"Viongozi wote hakikisheni mnahamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa ili watoto wapate mahali pa kusomea maana kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa," alisema.

Katika hatua nyingine, Halmashauri ya Mji wa Bunda, ilisema itahakikisha watoto wa marehemu diwani huyo wanapata elimu ikwa ni hatua mojawapo ya kumuenzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Abraham Mayaya, alisema wakati akielezea uadilifu na utendaji kazi mzuri wa diwani huyo kwa vipindi vyote alipokuwa mwenyekiti wa kamati ya maadili.

Naye mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bunda, Justine Rukaka, alisema pia chama hicho wilayani hapa, kitahakikisha kinachangia ili watoto hao kupata haki yao ya msingi ambayo ni elimu.

Hatua hiyo ilitokana na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Kiboye, kuwaagiza wahakikishe watoto wa marehemu wanapata elimu, huku naye akiahidi kufanya hivyo na kuungwa mkono na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Stephen Wasira.

Wasira alisema taasisi yake ya Wasira Foundation, inayotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni na kwamba itawasaidia watoto hao.

# Tigo yakabidhi kitita cha mil. 20/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imewatangaza washindi wa promosheni ya wakala kinara wa Tigopesa kitaifa na kikanda na mshindi wa kwanza amekabidhiwa zawadi ya milioni 20 baada ya kuibuka kidedea.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Tigopesa, Angelica Pesha, alisema promosheni hiyo ilifanyika kwa ajili ya kuwashukuru mawakala wake nchi nzima kwa kuwahudumia wateja.

Alisema shindano hilo ambalo liliendeshwa na kitengo cha Tigopesa kwa ajili ya kutoa shukrani kwa mawakala zaidi ya 100,000 waliopo nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwahudumia wateja.

Alisema shindano hilo lilianza rasmi Desemba Mosi na ilifikia kikomo Desemba 31, mwaka jana, lilishirikisha mawakala wa Tigopesa nchi nzima kwa kugawanywa kwa kanda.

Kanda zilizoshiriki kwenye shindano hilo ni pamoja na Pwani, Kaskazini, Kusini na Kanda ya Ziwa.

Alisema shindano lilianzia ngazi ya kanda na kila kanda walipatikana washindi wawili na baadaye wakapatikana wa kitaifa.

Angelica alisema zaidi ya Sh. milioni 50 zimeshindaniwa na washindi wa kanda wa kwanza alipata Sh. milioni tatu na wa pili Sh. milioni mbili na jumla ni Sh. milioni 20 zilishindaniwa.

Alisema Kampuni ya Tigo, imekuwa mstari wa mbele kwa ubunifu ikiwa ni pamoja na kuandaa promosheni mbalimbali na kuwashukuru wadau wao.

Aliwapongeza washindi wote nchini kutokana na kuibuka kidedea na wanatarajia kuendesha promosheni kila wakati.

"Kama kampuni kamili ya fedha, tumekuwa tukitoa huduma mbalimbali na tunawapongeza washindi wote waliojishindia zawadi hizo na tutaendelea kuwa wabunifu kila wakati," alisema.

Kwa upande wa mshindi wa kwanza wa Sh. milioni 20, Hajira Fadhil kutoka Ilala, alisema kuwa anaishukuru kampuni ya Tigo kutokana na kuendesha shindano hilo na kuibuka kidedea.

Alisema kuwa yeye ni mama wa watoto watano na anatarajia kutumia fedha hizo kwa ajili ya kufungua duka jingine la wakala wa Tigopesa ili kuhakikisha anakuza biashara yake.

Naye mshindi wa pili, Suleiman Hussein, kutoka Zanzibar, alisema amefurahia kupata ushindi na ana imani fedha hizo zitamsaidia kuendeleza na kuboresha huduma ya uwakala.

"Nimefurahia kupata ushindi wa pili kitaifa na kwamba ninatarajia kutumia fedha hizi kuendeleza na kuiboresha biashara yangu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


## CHETI KIMEPOTEA




115577802

**HASSAN MBWANA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0731/0469 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2005 kupitia MAKONGO SEKONDARI.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: DAR/KIJ/RB/25683/2020.**

## CHETI KIMEPOTEA



115577602

**PONSIAN G. MUSHI anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4827/0126 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2014 kupitia SAINT PETER CLAVER HIGH SCHOOL.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.**

**Taarifa ya polisi: UD/RB/2224/2019.**

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA
CIVIL APPEAL NO. 8/2018
JENITHA R. TIBIHENDA...............PLAINTIFF
VERSUS
NELSON A. MAKOTI & OTHERS...DEFENDANTS

TO: NELSON A. MAKOTI

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned appellant has logged a case registered as civil appeal No. 8 of 2018 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba. Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 22nd day of January, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge F.H. Mtulya. You are authorized to appear in person or through your advocate. Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 17th day of December, 2019.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

115577702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULMAJID OMAR AL BAKRY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 182 CAS TOYOTA CHASER.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/515890/2019.

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ALAM SIMBA YUSUPH**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 124 DBT, Aina yake NOAH Yenye chasis namba : SR40019849.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi:

Taarifa ya Polisi: MIK/RB/614/2016.

## VYETI VIMEPOTEA




115577102

GERALD SAMWEL anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0918-0068 kilichotolewa na KIMYAKI SEKONDARI mwaka 2008. Certificate in Cultural Heritage Management and Tour Guidance namba 2009-01-00557 cha DSM UNIVERSITY mwaka 2010. Diploma in Cultural Heritage and Tour Guidance namba 2010-02-00087 cha DSM UNIVERSITY mwaka 2011. Degree in Social Works namba BSWBIT.2012/62 cha CHUO CHA USTAWI WA JAMII mwaka 2015.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: IKW/RB/22/2020.

## KUPOTEA KWA CHETI



115577402

**MASUNGA SAYI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **Index No. S.0422/0082** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 1996 **HEDARU SEC SCHOOL** . Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye . TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/555246/2019**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;5/2020**

**Ombi la KUDRA RASHID MAUMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FATUMA ABDALLAH MSONGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/01/2020.

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115577502


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# PSG YAGOMA KUMWACHIA CAVANI




**PARIS,** Ufaransa

EDINSON Cavani anaangalia uwezekano wa kubakia Paris Saint-Germain baada ya kocha, Thomas Tuchel kubainisha hakutakuwa na wa kuondoka Januari hii, huku Leonardo akiripotiwa kutaka kumbakiza mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay.

Cavani mwenye umri wa miaka 32, yupo kwenye miezi yake sita ya mwisho kwenye mkataba wake na PSG na amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka baada ya kukosa nafasi, lakini sasa hilo linaonekana halitawezekana.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Leonardo amesema kwamba amemwambia Cavani kuwa hataruhusiwa kuondoka Januari hii, licha ya kuwasili kwa Mauro Icardi ambaye ni kama amepora namba yake kwenye kikosi cha kwanza na ameanza katika mechi nne tu za Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Napoliameripotiwa kwamba, anawaniwa na Manchester United na Arsenal, hata hivyo, inaonyesha kuwa atamalizia miezi yake iliyobaki hapo jijini Paris.

Wakati alipoulizwa kama amekubaliana na maamuzi ya Leonardo, Tuchel alisema: "Tunahitaji kufanya maamuzi magumu na sisi (Tuchel na Leonardo) tuna maoni sawa.

Lakini Tuchel alibainisha kwamba, fowadi huyo mwenye uzoefu atapigania kuhakikisha anapata namba kwenye kikosi cha kwanza.

"Inategemea na ubora wa wachezaji wengine na yeye pia," alisema Tuchel.

# Sissoko nje ya dimba miezi mitatu

**LONDON,** England

KIUNGO wa Tottenham, Moussa Sissoko, anatarajia kuwa nje ya dimba kwa angalau miezi mitatu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliamua wakati timu yake ikichapwa 1-0 na Southampton Januari Mosi kwenye mchezo wa Ligi Kuu na alikosa katika sare ya 1-1 dhidi ya Middlesbrough kwenye mchezo wa Kombe la FA Jumapili iliyopita.

Spurs inatarajia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kurudi kwenye mazoezi mwanzoni mwa Aprili mwaka huu.

"Baada ya kufanyiwa vipimo, Moussa Sissoko leo (juzi) amefanyiwa operesheni ya goti lake la kulia," taarifa ya Spurs ilisema.

"Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ufaransa aliumia wakati wa mchezo wetu dhidi ya Southampton, na matokeo yake akaukosa mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Middlesbrough.

"Timu yetu wa madaktari itakuwa ikimwangalia na kufuatilia maendeleo ya Moussa kabla ya kurudi kwenye mazoezi mwanzoni mwa Aprili."

Sissoko amecheza mechi 26 kwa Spurs katika mashindano yote msimu huu, akifunga kwenye ushindi wa mechi za Ligi dhidi ya Bournemouth na Burnley.

Majeruhi yake yanamweka kwenye shaka ya kuitwa kwenye kikosi cha Ufaransa chini ya kocha, Didier Deschamps kwa ajili ya michuano ya Euro 2020, huu mabingwa hao wa dunia wakianza mashindano hayo dhidi ya Ujerumani mjini Munich Juni 16, mwaka huu.







# Liverpool yampeleka Rhian Brewster Swansea

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Rhian Brewster amejiunga na Swansea City kwa mkopo kwa msimu wote uliobaki.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 amejiunga na kocha Steve Cooper, ambaye alikuwa kocha wake kwenye Timu Taifa ya England chini ya umri wa miaka 17 walipotwaa Kombe la Dunia mwaka 2017 na yeye alitwaa kiatu cha dhahabu kwa ufungaji bora.

Brewster ameichezea mechi tatu tu Liverpool msimu huu wa 2019-20, huku mchezo wa karibuni zaidi ni alipoingia akitokea benchi wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Everton kwenye mchezo wa Kombe la FA pale kwenye dimba la Anfield, Jumapili iliyopita.

Mshambuliaji huyo ataanza kuichezea timu yake hiyo mpya kwenye mchezo dhidi ya Cardiff City Januari 12.

# Zidane aelezea anavyomwamini Jovic

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amemwelezea Luka Jovic kama ndio mshambuliaji muhimu zaidi wa Real Madrid kwa siku za usoni, kabla ya mchezo wake wa Kombe la Supercopa de Espana, uliopigwa jana Jumatano.

Huku Karim Benzema akiwa majeruhi na Gareth Bale mgonjwa, Jovic ndio alikuwa akitegemea kuongoza safu ya mashambulizi ya Madrid kwenye nusu fainali ya kombe hilo la Hispania dhidi ya Valencia mjini Jeddah.

Ilikuwa hatua nzuri kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye alikuwa kwenye wakati mgumu kupata namba kikosi cha kwanza tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea Eintracht Frankfurt kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 60 Juni mwaka jana.

Jovic ameanza katika mechi nne tu za kimashindano chini ya Zidane, huku akiwa na bao moja alilofunga wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Leganes pale dimba la Santiago Bernabeu Oktoba 30, mwaka jana ukiwa ni mchezo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga.

Zidane aliripotiwa kwamba hajashawishika na kiwango cha Jovic, lakini wakati akizungumza na waandishi wa habari Jumanne, alielezea kuwa huyo ni mchezaji muhimu wa baadaye wa Madrid.

"Hisia ni nzuri, licha ya kukosekana mara kadhaa. Kuna kikosi kikubwa na wengine pia watapata nafasi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Jovic kwa hakika ni mbadala. Yeye ndio matarajio ya baadaye. Anatakiwa kutulia, anajifunza.

"Ni kijana ambaye anataka kujifunza mengi. Ni mtu mzuri. Hatafunga mabao mengi. Tumekuwa tukimuunga mkono na unatakiwa kutulia kwa ajili yake."






# SOLSKJAER: TULICHEZA OVYO KIPINDI CHA KWANZA

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anahisi kwamba, Manchester United walicheza vibaya zaidi kipindi cha kwanza kuliko siku nyingine yoyote msimu huu dhidi ya Manchester City kwenye nusu fainali ya kwanza ya EFL, juzi Jumanne.

City walitawala kipindi cha kwanza kwenye nusu fainali hiyo ya kwanza katika dimba la Old Trafford, ambapo Bernardo Silva na Riyad Mahrez kila mmoja alifunga bao kabla ya Andreas Pereira kujifunga.

Marcus Rashford alifunga bao la United kipindi cha pili, na kuwapa wao matumaini finyu kuelekea nusu fainali ya pili kwenye Uwanja wa Etihad Januari 29, mwaka huu wakiwa wanakwenda pale wakiwa nyuma kwa 3-1.

Solskjaer hakuwa na furaha na namna kikosi chake kilivyoanza kipindi cha kwanza, hasa baada ya bao la kwanza la Silva dakika ya 17.

"Kuanzia bao lao la kwanza hadi kipindi cha pili, tulicheza vibaya zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kabla ya hapo, tulicheza vizuri, bao moja, lakini kwa sasa haijalishi sana.

"Kwa sasa tunafikiria zaidi mchezo wetu wa Ligi Kuu Jumapili dhidi ya Norwich City. Baada ya kipindi cha pili tulipata kitu ambacho tunaweza kukiamini."

# Guardiola ahofia Utd kupindua meza

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amebakia akihofia Manchester United inaweza "kupindua meza" kwenye nusu fainali yao ya pili ya Kombe la EFL, licha ya Manchester City kupata ushindi wa mabao 3-1 katika uwanja wa Old Trafford Jumanne.

City walitawala zaidi kipindi cha kwanza wakati Bernardo Silva na Riyad Mahrez walipofunga na Andreas Pereira akajifunga.

Marcus Rashford alifunga la kufutia machozi kwa United, ambao watakwenda pale uwanja wa Etihad kwenye nusu fainali ya pili Januari 29 mwaka huu.


Lakini Guardiola alidokeza kwamba, namna United ilivyopindua meza dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakati walipokuwa nyuma kwa 2-0 nyumbani hatua ya 16 bora, wanaweza kufanya hivyo kwenye mchezo wao huo.

"Nimecheza mara nyingi dhidi ya United, sio tu hapa, lakini wakati nikiwa kule Munich na hasa pale Barcelona, na fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.


"Bila shaka nina heshima kubwa kwa klabu hii na historia yake," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Klabu hii imeisaidia Ligi Kuu England na Ulaya, kuufanya mchezo kuwa sehemu bora. Bila shaka ni hatua nzuri, na kujaribu kucheza vizuri kama tulivyofanya hapa.

"Lakini huu sio mchezo wa pointi tatu, kwa hiyo mambo hayajaisha. Msimu uliopita walifungwa 2-0 na PSG na walipokwenda Ufaransa na unajua kwamba walifuzu.

"Kitu chochote kinaweza kutokea kwenye soka."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANE MWANASOKA BORA AFRIKA 2019

## Ni mchezaji wa kwanza kutoka Senegal kushinda tuzo hiyo tangu 2002...

**CAIRO,** Misri

SADIO Mane alimshinda mchezaji mwenzake wa Liverpool, Mohamed Salah na nyota wa Manchester City, Riyad Mahrez kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka wa Afrika kwa mwaka 2019, tuzo inayotolewa na Shirikisho la Soka la Afrika (Caf).

**Mane alikuwa kwenye kiwango bora pale Liverpool kwa kutwaa taji la Ligi ya Mbingwa Ulaya na pia alianza vizuri msimu wa Ligi Kuu England mwaka 2019-20.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alimaliza nafasi tatu kwa miaka mitatu iliyopita, akimaliza nafasi ya pili nyuma ya Salah mwaka 2017 na 2018, na nafasi ya tatu mwaka 2016 wakati Mahrez aliposhinda.

Lakini wakati huu Mane aliitwaa tuzo hiyo, mbele ya mchezaji mwenzake wa Liverpool, Salah na Mahrez, ambaye alitwaa mataji matatu ya nyumbani na City na alikuwa nahodha wa Algeria wakati ikitwaa taji la Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka jana huko nchini Misri.

Hii ni mara ya kwanza tangu mwaka 2002 kwa mchezaji wa Senegal kutwaa tuzo hiyo, straika wa zamani wa Liverpool, El Hadji Diouf ndio alikuwa mchezaji wa mwisho kutwaa tuzo hiyo muda mfupi baada ya kuondoka Lens kwenda Liverpool.

Wakati mafanikio ya Liverpool kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya bila shaka yoyote yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na Mane, pia alifurahia mwaka mzuri kwa upande wake.

Katika mechi 36 za Ligi Kuu England aliyoichezea mwaka 2019, Mane alifunga mabao 24 na kutoa 'asisti' sita na kumwacha Salah (mabao 18 na 'asisti' tano kwenye mechi 34) wakati Mahrez alifunga mabao saba na 'asisti' saba katika mechi 24 alizoshuka dimbani.

Mane, Salah na Mahrez pia walitajwa kwenye kikosi bora cha mwaka cha Caf. Pierre-Emerick Aubameyang alichaguliwa kuwa ndio mshambuliaji kiongozi wa kikosi hicho, huku Hakim Ziyech na Idrissa Gueye wakichaguliwa nafasi ya kiungo na Andre Onana akiwa golini.

Kalidou Koulibaly, Joel Matip, Serge Aurier na Achraf Hakimi - ambaye alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka kijana, wamechaguliwa nafasi ya ulinzi na Djamel Belmadi wa Algeria alichaguliwa kuwa kocha bora wa mwaka.

## ZISIKUPITE

### ZAHA AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA imeweka wazi nia yake ya kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha katika dirisha dogo la Januari, lakini haina uwezo wa kulipa ada ya pauni milioni 80 ambayo imetajwa na klabu yake hiyo maarufu Eagles. ***(Express)***

### ADA KUMWAMISHA ZAHA

WAKALA wa mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, amesema anataka kuona mchezaji wake huyo mwenye umri wa miaka 27, anajiunga na Tottenham Hotspur, lakini klabu hiyo pia imeweka wazi haina uwezo wa kulipa kiasi cha ada kinachotakiwa. ***(Mirror)***

### TRAORE ATAJWA CITY

MANCHESTER City imesema inahitaji kumsajili winga wa Wolves Mhispania Adama Traore, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Calcio Mercato)***

### VIDAL AKARIBIA UNITED

WAKALA wa kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal (32), anatarajia kufanya mazungumzo na Manchester United kuhusu uwezekano wa nyota huyo kujiunga na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Corriere Della Sera, via Mirror)***

### VILLA KUMREJESHA BENTEKE

ASTON Villa imeanza mazungumzo na Crystal Palace kwa ajili ya kumrejesha straika wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Christian Benteke, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Telegraph)***

### REINA AKARIBIA VILLA

MABOSI wa Aston Villa wamewasilisha taarifa rasmi ya kumwania golikipa wa zamani wa Liverpool, Mhispania Pepe Reina (37), kutokea AC Milan. ***(Mail)***

### ALONSO KUTUA INTER

BEKI wa kushoto wa Chelsea, Marcos Alonso anatajwa kuwindwa na Inter Milan ya Italia huku The Blues ikiwa tayari kumwachia nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania mwenye umri wa miaka 29. ***(Telegraph)***

### SIGUEDSSON KUTEMWA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Iceland, Gylfi Sigurdsson (30), ni mmoja wa wachezaji ambao Kocha wa Everton, Carlo Ancelotti, anatarajia kuwaacha kwenye kikosi chake. ***(Sun)***

### RABIOT ANUKIA EVERTON

EVERTON imeweka wazi nia yake ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, ambaye ana umri wa miaka 24, ili kuitumikia klabu hiyo hadi mwisho wa msimu. ***(Corriere Dello Sport, via Sport Witness)***

### GOTZE KUONDOKA DORTMUND

NYOTA Mario Gotze, ambaye alifunga bao la ushindi kwa Ujerumani katika fainali za Kombe la Dunia mwaka 2014, anatarajia kuondoka Borussia Dortmund akiwa mchezaji huru ifikapo mwishoni mwa msimu huu. Mshambuliaji huyo aliwahi kufundishwa na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola na Jurgen Klopp wa Liverpool. ***(Bild - in German)***

## Mkwasa atakiwa kupumzika Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA kiungo tegemeo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mtemi Ramadhani, amemshauri Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, kuachana na timu hiyo kwa maslahi ya afya yake.

Hata hivyo, siku moja kabla ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga, Mkwasa alikaririwa akisema afya yake iko vizuri baada ya kupona maradhi ya moyo yaliyokuwa yanamsumbua.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtemi alisema kazi ya kufundisha mpira wa miguu inazungukwa na mazingira ya presha na ili kutompa wakati mgumu, Mkwasa anatakiwa kukaa pembeni ili kulinda afya yake.

Mtemi alisema kuwa Yanga inatakiwa kusaka kocha mwingine wa kudumu na jukumu la Mkwasa ni kuwavusha katika kipindi hiki walichokuwa na changamoto.

"Mimi Mkwasa ni rafiki yangu, tunakituo kimoja ambacho tunakisimamia, najua ni mgonjwa, kitendo cha kutolewa moyo na kuwekwa mezani ili kutibiwa si kidogo, anahitaji kukaa kwenye mazingira ya utulivu, si ya kufundisha," alisema nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Mkwasa alitua Yanga kuchukua mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera ambaye alitimuliwa na uongozi wa timu hiyo Novemba mwaka jana.

## Usajili Zanzibar kufungwa rasmi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema dirisha dogo la usajili wa wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Visiwani hapa litafungwa rasmi leo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada alisema dirisha hilo litafungwa saa 12: 00 jioni na linawakumbusha viongozi wa klabu hakutakuwa na muda wa nyongeza.

Ahmada alisema kuwa wanazitaka klabu kuhakikisha wanakamilisha taratibu zote za usajili ili kuondoka usumbufu wa kushindwa kuwapata wachezaji iliyowaongeza.

"Ni vyema vilabu vikarejesha fomu kwa wakati uliopangwa ili kuondoa usumbufu ambao mara kwa mara umekuwa ukijitokeza wa kwa baadhi ya vilabu kuchelewa kurejesha fomu hizo.

"Zoezi limeenda vizuri, licha ya baadhi ya vilabu kufanya usajili katika tarehe za mwishoni kabisa hali ambayo inasababisha hata baadaye kuchelewa kurejesha fomu hizo na kutegemea kulipa faini," alisema kiongozi huyo.

Hata hivyo alizitaka timu kuzingatia kanuni za mashindano kwa kumalizana na wachezaji ambao imefikia uamuzi wa kuwaacha.

# KOCHA JAMHURI AFAFANUA YANGA ILIPOWAZIDI NGUVU

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

LICHA ya kukubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Yanga, Kocha wa Jamhuri, Mustafa Hassan maarufu 'Mu', amesema mfumo walioutumia katika mchezo huo wa Kombe la Mapinduzi, umewaepushia balaa la kufungwa mabao mengi.

**Yanga juzi usiku ilitinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi baada ya kuibuka na ushindi katika mechi iliyopigwa kwenye Uwanja wa Amaan.**

Mabao ya Yanga katika mechi hiyo yalifungwa na Adeyum Saleh dakika ya 45 na mtokea benchi, Mohamed Isssa 'Banka' dakika ya 85.

Kwa matokeo hayo sasa Yanga itakutana na Mtibwa Sugar leo saa 2:15 usiku katika mchezo wa nusu fainali utakaopigwa kwenye Uwanja wa Amaan, Unguja.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Mu alisema kwa sasa Yanga imeimarika sana katika eneo la kiungo cha kati na ndiyo idara iliyowapa sana tabu.

Alisema kama wangecheza mchezo wa wazi 'wangepigwa' mabao mengi zaidi kutokana na ubora mkubwa wa wapinzani wao.

"Kila Yanga ilipofanya 'sub' (mabadiliko) hali ilizidi kuwa mbaya zaidi kwetu na kama tungecheza 'free game', tungepigwa mabao mengi," alisema.

Aidha, alisema kitendo cha wachezaji wake kucheza na jukwaa ni moja ya tatizo lililoigharimu timu yao na kuchangia kipigo hicho juzi.

Fainali za mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka inatarajiwa kuchezwa Januari 13, mwaka huu kwa bingwa kuondoka na kitita cha Sh. milioni 15.



Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Vijana Kids, Amim Jamhuri, akifunga bao licha ya kukabwa na wachezaji wenzake wa timu hiyo katika mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Jakaya Mrisho Kikwete (JMK Park) jijini Dares Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Banka afunguka kasi ya kutupia*

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAKATI akitarajiwa kuibeba tena timu yake itakaposhuka dimbani dhidi ya Mtibwa Sugar leo, kiungo mshambuliaji wa Yanga, Mohamed Issa 'Banka', ametoa siri ya kuendelea kucheka na nyavu.

Banka amefunga mfululizo wakati huu akitokea chumba cha majeruhi, ambapo kabla ya juzi kutupia dhidi ya Jamhuri kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi, pia alifunga dhidi ya Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Bara.

Katika mechi hiyo ya juzi iliyopigwa Uwanja wa Amaan na Yanga kushinda 2-0, Banka alitokea benchi kipindi cha pili na kutupia dakika ya 85 baada ya Adeyum Saleh kutangulia kuziona nyavu dakika ya 45.

Akizungumza na Nipashe visiwani hapa, Banka alisema huu ni wakati wa mashabiki wa Yanga kufurahia matunda yake baada ya kumvumilia kipindi akiwa majeruhi.

"Siri kubwa ya mafanikio haya ni mazoezi na kujituma, lakini pia ushirikiano mkubwa ninaopata kutoka kwa wachezaji wenzangu.

"Nawaomba mashabiki wa Yanga waendelee kutuunga mkono watafurahia ubora wetu katika mechi zinazofuata," Banka alisema.

Akizungumzia mchezo wa nusu fainali leo dhidi ya Mtibwa Sugar, alisema utakuwa mgumu kwa kuwa ni timu inayowafahamu vizuri.

"Mtibwa tunacheza nao ligi moja na ni timu bora, hautakuwa mchezo mwepesi, lakini tumekuja kupambana," alisema.

Michezo

Alhamisi Januari 9, 2020
Nipashe




Mane Mwanasoka Bora Afrika 2019

HABARI UK.30



Mshambuliaji wa Manchester City, Riyad Mahrez (kulia), akifunga bao la pili kwa timu yake huku golikipa wa Manchester United, David de Gea akishindwa kuokoa hatari hiyo katika mechi ya Kombe la Ligi iliyochezwa juzi, usiku kwenye Uwanja wa Old Trafford. City ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Yanga zazifuta Azam FC, Mtibwa Z'bar

## Mashabiki waziombea zitinge fainali washuhudie 'dabi', Bocco na Banka watoa neno...

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

BAADA ya Yanga juzi usiku kuungana na Simba, Azam FC na Mtibwa Sugar kutinga nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi habari ya mjini visiwani hapa sasa ni 'dua' kwa timu hizo kongwe nchi kukutana fainali.

**Yanga imetinga nusu fainali baada ya kuichapa Jamhuri kwa mabao 2-0 yaliyowekwa kimyani na Adeyum Saleh na Mohamed Issa 'Banka' dakika ya 45 na 85 kwenye Uwanja wa Amaan juzi usiku.**

Wakati Simba yenyewe ikitinga nusu fainali juzi jioni kwa kuichapa Zimamoto 3-1 shukrani kwa mabao ya John Bocco, Sharaf Shiboub na Ibrahim Ajibu.

Kwa upande wa Azam na Mtibwa zilizitoa Mlandege na Chipukizi kwa ushindi wa 1-0 na mikwaju ya penalti 4-2 baada ya sare bao 1-1.

Hata hivyo, wakati Yanga ikishuka dimbani leo saa 2:15 usiku kuvaana na Mtibwa Sugar katika nusu fainali ya kwanza kabla ya Simba kesho majira kama hayo kuvaana na mabingwa watetezi, Azam FC mashabiki visiwani hapa maombi yao ni kuona watani hao wa jadi wakikutana fainali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya Yanga kutinga nusu fainali, waliliambia Nipashe kuwa wanatamani kuona Mtibwa na Azam zikitolewa ili washuhudie 'dabi' ya watani hao.

Kocha wa Jamhuri, Mustafa Hassan 'Mu', baada ya timu yake kuangukia kipigo, alisema anaziona Simba na Yanga zikitinga fainali ingawa mpira ni dakika 90 na lolote linaweza kutokea.

"Wapenzi wengi wasoka wanataka Simba na Yanga zikutane fainali, jambo ambalo hata mimi natamani hivyo, lakini ukumbuke Azam ni wazoefu wa michuano hii na wapo vizuri wakitaka kutetea ubingwa wao.

"Ila tofauti na miaka mingine mwaka huu naona Simba na Yanga zimedhamiria ubingwa na zimeleta vikosi kamili, nadhani zinaweza kukutana," alisema.

Nassor Juma, mdau wa soka ambaye hakuwa tayari kueleza yeye ni shabiki wa timu ipi kati ya Simba na Yanga, alisema: "Ni wakati wa Wazanzibar kushuhudia dabi kwenye Uwanja wa Amaan, hivyo dua zangu Azam na Mtibwa zitolewe."

Straika wa Yanga aliyerejea katika makali yake akitokea chumba cha majeruhi, Banka alisema hesabu zao kwanza ni kwa Mtibwa na hawaihofii timu yoyote.

"Simba tumekutana nayo wiki iliyopita, hatuna hofu tumekuja kupambana na lengo letu ni kutwaa kombe tupo tayari kucheza na timu yoyote," alisema.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Kocha msaidizi wa Yanga, Said Maulid aliyepo visiwani hapa na timu, ambapo alisema mechi zote ni ngumu lakini walichofuata ni kombe hivyo wapo tayari kukutana na Simba kama ikitokea.

Kwa upande wake nahodha wa Simba, John Bocco, alisema wamekuja kupambana na wanatambua Azam ni timu kubwa lakini wanachotaka ni kombe tu.

Alisema baada ya kulikosa kombe hilo mwaka jana kwa kupoteza mechi ya fainali dhidi ya Azam, safari hii hawataki kurudia makosa hayo tena.

## Msuva afurahia ndoto zimetimia

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, amesema ndoto zake za kucheza soka la kulipwa Ulaya zimetimia baada ya kukamilika kwa 'dili' la kujiunga na klabu ya Benfica ya Ureno.

Msuva amesaini mkataba wa miaka mitatu wa kuichezea timu hiyo lakini atapelekwa kwa mkopo wa miezi sita katika timu ya Pananthiakos.

Akizungumza na Nipashe jana, Msuva, alisema kuwa juhudi na bidii zake ndio zimefanikisha usajili huo na anaamini ataendelea kucheza soka la ushindani na kiwango cha juu ili kujiongezea thamani yake.

Msuva alisema kuwa anamshukuru Mungu kwa kufika hatua hiyo, kwa sababu hakuna kinachowezekana bila ya kuwapo kwa mipango mizuri.

"Nina furaha sana, ndoto zangu za kucheza Ulaya, kusajiliwa na klabu kubwa zimetimia," alisema kwa kifupi mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga.

Meneja wa mchezaji huyo, Dk. Jonas Tiboroha, alisema kuwa Msuva anatarajiwa kutua Ureno ifikapo Januari 15, mwaka huu.

Yanga ilimuuza Msuva kwa Difaa El Jadida ya Morocco kwa dau la Dola za Marekani 100,000 mwaka 2016, lakini klabu hiyo ilikataa kuweka kipengele cha kulipwa fedha endapo atauzwa kwa timu nyingine.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >